# Watu wana uliza maswali,

# Mungu anajibu

# Kupitia NENO LAKE

**Imefanywa na**

**Mishonari**

**Ewald Frank**

Mwandishi Yule Yule ameandika kuhusu masoma ya muhimu ambazo maandiko matakatifu yana zungumzia. Brosha hizi zinasambazwa duniani pote katika lugha nyingi tofauti nazimekuwa Baraka kwa watu wengi.
Hapa kwenye kituo cha misheni tu natangaza pia mahubiri za Ndugu Branham iliyo hariliwa yanayo tumwa kutokana na ombi la wale wanao itaji kuipata. Orodha ya yavitabu vilivyo chapwa inaweza kupatiliwa.
Waweza kushangazwa na kujuwa nichakula chakiroho ghani ambacho BWANA mupendwa na mukombozi alicho tayarishiya walio wake.
Ikiwa unapendezwa unaweza kuandika kupitiya anuwani hii ifwatayo.


Kituo cha Misheni
Sanduku la Posta 100707
47707 Krefeld
Ujerumani

Simu: +492151545151
Fax: +49-2151/951293

Barua pepe: volksmission@gmx.de or
E. frank@freie-volksmission.de

Ukurasa wa vuti: http://www.freie-volksmission.de



Mwandishi na mchapishaji E. Frank

*******

Septemba 2006

# MASWALI ZILIZO WEKWA MBELE YA NDUGU EWALD FRANK KUTOKA KWA WA HUDMU WA INCHI TOFAUTI

> *Tena haimpasi mtumwa wa Bwana kuwa mgonvi; baali kuwa mpole kwa watu wote, awezae kufundisha, mvumilivu; akiwaonya kwa upole wanaoshindana naye, ili kama ikiweza kana Mungu awape kutubu na kuijua kweli; wapate tena fahamu zao na kutoka katika mtego wa ibilisi, ambao hao wametegwa naye hata kuyafanya mapenzi yake.* (2. Timotheo 2:24-26)
>
> Kwa ufafanuzi huu tuna shughulika na Uzima na kifo. Katika Neno muna Uzima, katika matafsiri muna kifo. Kila tafsiri ni mtego ambao adui anaweka kwenye shingo la watu. Yeye si kila wakati hakazi pua mara moja, lakini anaacha watu wale wakiwa wafungwa na kuwafanya watumwa wa mapenzi yake, kama vile andiko lilianza onesha wazi wazi.

Tangu nilipo kuwa katika kazi ya Mungu kwa nusu karne ni mewekwa ndani tumaini na wandugu katika hudma ulimwenguni pote kwa neema ya Mungu. Walitambua kwamba Mungu aliniweka ili kuchukuwa injili ya milele katika mataifa yote ya ulimwenguni. Baada ya hudma ya Ndugu Branham ni uajibu wangu wa kugawa Neno la kweli la Mungu pamoja na watu wa Mungu pamoja na watumishi wote waaminifu kama vile ilivyo kuwa katika siku za BWANA wetu na nyakati za kimitume na manabii,ndivyo pamoja na Ujumbe leo, *"… katika nyaraka hizo yamo mambo ambayo ni vigumu kuelewa nayo; na mambo hayo watu wasiyo na elimu, wasio imara, huyapotoa kama vile waya potoavyo na maandiko mengine kwa uvunjifu wao wenyewe"*(2. Petro 3:16). Hivi ndivyo imekuwa katika nyakati zote. Matafsiri tofauti yame sababisha magawanyiko mengi, na muvurugano wa kimafundisho, na hata katika ujumbe wa wakati. Wahudmu wanaohusika kikweli na mambo ya kiroho ya watu wa Mungu, hawana haja tena ya kukubali hali ya sasa na wanauliza ufafanuzi kuhusu mambo mbali mbali. Watoto wa kweli wote wa Mungu wana haki na itaji yakujua majibu yaliyo ya kweli yanayo simamia kwa ukweli wa maandiko matakatifu. Nili mjua Ndugu Branham kipekee na mimi ni mushuda wa hudma yake ya kimaajabu.

Kwa mwezi wa Ogasti,1955 nilihuzuria mikutano yake kwa juma yote. Kutoka Septemba 1958, nili anza kupokea makanda za mahubiri aliyo ya hubiri huko Marekani kupitia Baruwa na kuanza kuzitafsiri katika lugha ya Kijerumani kwa mara na mara. Kwa Disemba, 1962, nilipo kuwa na mazungumuzo ya kipekee na Ndugu Branham, nili mueleza namna ninavyo fanya hii, ni lipo tumikisha vifaa vya kichwa kwa kusikiliza mahubiri na kuyatafsiri katika lugha ya Kijerumani kwa ajili ya mukutano uliyo kusanyika. Kwa mwaka wa 1963 alikumbuka hii na kuliongelea,

"Hudma ya kanda ni jambo la ulimwengu, mahali pote. Nafikiri kwamba hiyo ninjia ambao Mungu amepata kwa ajili ya kusambaza ujumbe kwenye ardhi za mataifa hapo nyuma, na kurudishwa mahali linastahili kutafsiriwa katika Ujerumani. walipata makanda, kwenye makundi zao za mamia na mamia za watu; wanaweka vitu kidogo kwenye masikio yao, wana weka kanda. Kama vile ninavyo ongea muhudmu anasimama hapo na kufanya sawasawa, katika lugha nyingine, na kuileta mbele ya mamia. Na mamia wanaokoka na kupona kupitia kwa njia ya makanda zinazo zunguka ulimwenguni. Yote katika kingereza, lakini zinatafsiriwa katika lugha nyingi, tofauti (Ulaya) katika makabila (Afrika ya kusini) duniani pote. Tuna sikia kutoka wao, nyuma hapo kupitia Barua pepe" (Ushuhuda, Shreveport, LA, V-17-N-5; Alhamisi, 63-11-28). Ni wazi kwamba ndugu Branham alikuwa akisema kuhusu kwa ndugu Sidney Jackson katika Afrika ya kusini na kwangu, kwamba sisi pekee ndiyo tulikuwa tukitafsiri mahubiri yake kwa wakati huo.

Katika myaka makumi ine na saba iliyo isha, ni lisoma na kusikiliza mahubiri yake maranyingi na kuzitafsiri, hapo sasa nina weza kusema ya kwamba ninajua Ujumbe wa wakati wa mwisho kuliko wengine wote. Nimekuwa karibu sana pamoja na Neno la Mungu, maandiko matakatifu, tangu siku za ujana wangu. Kwa kweli ni wa chungaji wachache wanao uliza"Maandiko yana sema nini?". Wakati wanapo ni uliza maswali hizi wana nijalia, kwa kuwa majibu ni nazo zitoa nilazima ziwe zikilingana na maaandiko ya Neno la Mungu, ambayo ina dumu milele (Isaya 40:8, 1. Petro 1:23).

Swali 1a 1: Musimamo wako ni gani kuhusu hudma ya Ndugu Branham?

Swali la 2: Nimaneno gani halisi iliyompewa Ndugu Branham kwa utume wake?

Swali la 3: Maoni yako ni gani kuhusu Ujumbe wa wakati wa mwisho?

Swali la 4: Jee, unamkosoa Nabii kwa jambo Fulani?

Swali la 5: Yakini yako ni gani, Biblia ao Ujumbe?

Swali la 6: Jee, unafundisha tofauti na yale ambayo Ndugu Branham alifundisha?

Swali la 7: Jee, unaami kufunuliwa kwa mihuri saba?

Swali la 8: Muhuri wa saba Umefunuliwa?

Swali la 9: Unaamini ya kwamba Ufunuo 10:1-7 ilitimia kwa mwaka wa 1963?

Swali la 10: Unaamini ya kwamba ngurumo saba zime funuliwa kwa Ndugu Branham?

Swali la 11: Kwa nini Ndugu Branham aliongea mara nyingi kuhusu"Mvuto wa Tatu"?

Swali la 12: Kwanini Ndugu Branham mara nyingi alijilinganisha na Ufunuo 10:7?

Swali la 13: Unaamini hudma ya mujumbe wa munane?

Swali la 14: Unaami fundisho la Parousia?

Swali la 15: Jee, mwana wa Adamu kulingana na Luka 21:27, amekwisha kuja?

Swali la 16: Nivipi na hudma yako, imeshuhudiwa katika Biblia?

Swali la 17: Jee, unahubiri mahubiri ya Ndugu Branham?

Swali la 18: Chakula chakiroho ni gani, Je ni mahubiri ya Ndugu Branham ao Biblia?

Swali la 19: Ninani atakae lionyesha kanisa la wa wakati wa mwisho kwa BWANA?

Swali la 20: Unajikamata namna gani kwa wale wanao zihaki jina lako?

Swali la 21: Jee, Ndugu Branham alifundisha kuowa wake wengi?

Swali la 22: Unafundisha je kuhusu ndoa na talaka?

Swali la 23: Jee, ni vipi kuhusu yale yanao husu familia ya mutumishi wa Mungu?

Swali la 24: Ninamna gani kuhusi “Kitabu cha Nyakati saba za kanisa“?

Swali la 25: Jee, Muda za Nyakati za kanisa zilimfunuliwa Ndugu Branham?

Swali la 26: Jee, Ndugu Branham alitabiri kwamba mwisho wa Dunia ni katika waka 1977?

Swali la 27: Jee, Ndugu Branham aliona kalenda inayoisha kwa mwaka wa 1977?

Swali la 28: Jee, ubatizo wa Roho mtakatifu ni sawa sawa na kuzaliwa upya?

Swali la 29: Ni vipi kuhusu ano La Ndugu Branham katika hema?

Swali la 30: Jee, kitu chochote kilicho onyeshwa katika ono chaweza kubaki pasipo utimilifu?

Swali la 31: Twaweza kulinganisha namna gani kati ya Israeli na Kanisa?

Swali la 32: Kulingana na mpango wa Okuvu tuko katika sehemu gani?

Wandugu wapendwa katika BWANA,
Watoto wa Mungu wapendwa,

Ningependa ni seme wazi wazi ya kwamba: Hairuhusiwe kuweka fundisho yenye inasimamia kwa andiko moja la kibiblia, ao Msemo moja ya BWANA wetu, ao Nabii ao mtume. Ni lazima mbele ya Mungu, kwamba Neno lolote, lina pashwa kusimamia kwa ushuhuda wa watu wawili ao tatu, ao kwa ushuhuda mbili ao tatu ya maandiko ya kibiblia (Kumbukumbu 19:5). Hatuna injili moja tu, ila injili ine zinazo jazana moja kwa nyingine. Kwa mfano mtu asiye weza chukuwa utaratibu ya utume kwa ujao wake ginsi inavyo andikwa katika Mathayo 28:18-20, Marko 16:15-20, Lk 24:33-53, na Yohana 20:19-31, kwa ujao. Hapo kama mutu hatachukuwa hiyo hatimize utume wake kwa ujao. Na mwenye haongeze kwa hii utaratibu wa utume, Matendo 2:38 hata na maandiko nyingine yanayo onyesha namna gani hii inapashwa fanyi-

ka, naye hana ujao kwa uwingi kuhusu jibu la kweli kuhusu ubatizo wa kweli katika maji. Yeyeto anaye itajikujua kila kitu kuhusu kuzaliwa, Maisha, hudma, mateso na kifo, pia na hata kuhusu ufufuko na Kupanda mbiguni kwa BWANA wetu, na mkombozi anastahili kusoma hizo injili 4 zote. Na mwenye anataka kujua ya kwamba baada ya Ufufuko wa BWANA wetu ginsi alifundisha wanafunzi wake muda wa siku makumi ine kuhusu ufalme wa mbingu mbele ya kupanda kwake mbinguni, naye anapashwa soma matendo 1:1-3. Hapo tunakuta mambo ambayo haiku semeka katika injili ine: kwa mfano kwamba wakati alipanda mbinguni wingu lili mpokea (Matendo 1:9) kwa shahili 11, tunaambiwa kwamba atarudi akivaa mwili vilevile ginsi alivyo kwenda mbinguni (Luka 24:50-51). Katika 1. Yohana 3:2 inasemeka: *„…tuta fanana naye kwa maana tutamwona ginsi alivyo“*. Amena.

Yeyeto anaye kuwa naitaji ya kuelewa kuhusu kugeukia kwa Paulo kwa utume wake na hudma yake, hapashwi kusoma Matendo 9 pekee yake, ila ina mbidi tena kusoma na sura 22 na 26 ili aweza kuelewa tena zaidi. Anapashwa soma tena 1. Wakoritho 15:1-11 kwa sababu hakukuwa Petro baali alikuwa Paulo ambae alie onyesha kwamba baada ya ufufuko wa BWANA Yesu alionekana kwa wandugu zaidiya 500 kwa wakati moja kutoka mifano hizo tunao na vema kwamba haitoshi kutumia tu andiko moja, baali tunaweza kuongezea maadiko mengine yote ambayo yana husika na somo hiyo.

Maonyo haya onekani tena katika 2. Wakoritho 11:1-4, akisema kwamba wakati shetani, nyoka wa kale alimushawishi Hawa (Mwanzo. 3:1); aliongeza neno moja kwayale ambao BWANA Mungu alikuwa ameagiza Adamu, neno“hamta“hivyo ndivyo alivyo leta Hawa chini ya ushawishi wake wa hapohapo, na akageuka kuwa mfugwa wa mapenzi yake. Adui kila wakati analetaka mabishano kuhusu neno ambaye BWANA alisemaka mbele, lakini na hawezi kushika neno hilo na hawezi kudumu katika kweli ya Neno la kimsingi. Mungu alikuwa amesema *“Utakula miti yote ya Bustani kwabure…“* Adui alipanda mashaka akisema: *„Nini, Mungu alisema, msikule mti yote ya Bustani?“*

Hiyo neno moja iliyo ongezwa kwa yale ambayo Mungu alisema ndiyo ilikuwa sumu ya kidonda cha nyoka. Hapo ndipo ndoa ya kwanza ya kimwanadamu ilivyo achiliwa kwenye mauti, na kutengwa na Mungu. Kwanza ni mwana wa mtu anaye panda Mbegu njema ya Neno la Mungu badaye adui anafwata nyuma akipanda mbengu mbaya kupitia matafsiri (Mathayo 13). Hivyo ndivyo anavyo shika watu mateka na

kuwa weka chini ya mapenzi yake. Hii ndiyo wakati ya watu ya Mungu kufunguliwa kutoka katika mitego ya Yule adui na kurudishwa katika mapenzi ya Mungu. Upotevu yoyote inayo aminiwa inatokana na Neno ambalo linalo ongezwa kwa maandiko na kuligeuza, na kulitafsiri vibaya. Nandio sababu ya arifa hii inayo omba kushika kwa makini ya kutoongeza chochote ama kupunguza chochote kwa maneno ya unabii wa kitabu hiki (Ufunuo 22:18-19). Kama sivyo matokeo ya hiyo itaendelea kuwa upotevu.

Kwa kila swali la Kibiblia na kwa kila somo, kuna jibu moja tu la kweli linalo patikana katika maandiko inayo husu. Matafsiri tofauti nikazi ya adui-matokeo ya kula ku muti wa kujua mema na mabaya. Jambo hiyo moja imegusa kwa uwingi wa watu na mafundisho tofauti yenye inapati kana katika ya Ujumbe wa wakati wa mwisho. Kama tuna weza rudisha kila kitu kwenye maandiko matakatifu tuta kutana humo jibu moja ya kweli, na kutoelewa kutaisha. Angalisho ni kwa wa hudmu na makutano yote wanastahili kuwa macho na kurudi kwa hatua moja kwa heshima yote kwa neno la Mungu, lililo yakini ya mbingu na dunia. Katika mahubiri marefu ya Ndugu Branham ambayo aliyo hubiri“ Neno lililo nenwa ndiyo mbegu halisi“ya siku (Machi, 18, 1962), ambaye sisi wote tulisikiliza zaidi ya saa sita, tuna ona ginsi mtu wa Mungu alipatia utawala Neno la Mungu. “*…ikiwa hawa semi sawa sawa na neno hili, bila shaka kwa hao hawana asubui“* (Isaya. 8:20).

Tuna kubalishwa kwamba kuna masomo magumu katika Neno la Mungu, na hata pia katika Ujumbe, masomo ambayo tunastahili kuweka katika utaratibu wa Kimungu. Kwa mufano, wakati BWANA wetu alisema: *„…kwa maana hamtaimaliza miji ya Israeli, hata aja po mwana wa Adamu“* (Mathayo 10:23). Alisema tena*“Akawaambia, amina, nawa ambia, pana watu katika hawa wasimamao hapa ambao hawataonja mauti, hata wata kapo uona ufalme wa Mungu umekuja kwa nguvu“* (Marko 9:1). Tuna stahili kuangalia maneno haya katika mahali pake katika mupango wa okovu kwa utimilifu wake. Torati na manabii zilikuweko mpaka Yohana (Luka 16:16), tangu wakati huo ndipo ufalme wa Mungu ulihubiriwa. Siku ya pentekoste ufulme huo ulishuka na nguvu, kama vile ilivyo kuwa imetangazwa na Yohana mbatizaji katika Mathayo 3:2 na BWANA wetu katika Mathayo 4:17: Tangu wakati huo kanisa lilizaliwa na lilipokea maisha ya kiroho, na Mkombonzi alie tukuzwa alitembea katikati yao. Katika Ufunuo 1.

Yohana aliona Mwana wa Adamu katika kanisa lake, akionyeshwa kwenye vinara saba vya taa.

Kwa wa kati wake Paulo alijiweka ndani yeye mwenyewe akisema, *„Angalieni, niwaambia ninyi siri; hatuta lala sote, lakini sote tuta badilika.“* (1. Wakoritho 15:51). Sasa tunangoja utimilifu. Mtume Petro alipana arifa ya kutochanganya maandiko na masemi ya Mtume Paulo, akisema kwamba kuna mambo mengi yaliyo magumu kuyaelewa (2. Petro 3:15-16). Hakuna mtu anaye ruhusiwa kutafsiri na kufanya fundisho kwa yale maneno Ndugu Branham yaliyo kuwa magumu kuyaelewa. Alisema, kwa mfano, „Baada ya kuvunjwa kwa mihuri na siri itafunuliwa, Malaika akashuka, mjumbe, Kristo, na akaweka mguu yake juu ya nchi na Bahari na akiwa na upinde juu ya kichwa chake. Sasa, kumbukeni, huyu Malaika wa saba iko duniani kwa wakati wa kuja kwake“. Ndugu Branham alipokuwa duniani, ndipo „Malaika wa agano“alijifunua yeye mwenyewe katika wingu kubwa la kimaajabu. Nukuu: *„Huyo Malaika mkuu wa Agano, Yule alikuwa pamoja na Musa jangwani Yule alie mkuta Paulo katika njia ya kwenda Damasiki, aliruhusu picha yake iweze kushikwa nasi; Yule alieonekana katika picha ya «Life Magazine» iliyo tangaza. Ni ile neno ya Yule Mungu“* (Kristo ndiye siri ya Mungu iliyo funuliwa (Pg 92).

Alisema tena**: „Nahapa anarudi kwa sura ya 10 baada ya kuja kwake...“** Neno hili lamaanisha nini *„Baada ya wakati wa kuja...“* inalinganisha kuja kwa aina gani? Na inamaanisha nini na *„anakuja kwa sura ya 10 baada ya wakati wa kuja“* na mengineyo? Kwa dakika kidogo nyuma, Ndugu Branham alisema: „Amechukuwa Bibi arusi mtaifa na atamuchukuwa kwa nyumba ya mufalme, kwa nyumba ya baba yake katika utukufu, kwa ajili ya ndoa na sasa atashuka akija kujionyesha kwa wandugu wake 144, 000“. Enyi wahubiri na wa sihi ili mufanye angalisho kuhusu masemi haya, muya weke kwa nafasi inayo stahili kulingana na yale matukio na wakati yazo, na muache kuleta maoni yenu binafsi!kwa maana hakuna andiko ao fundisho la Mtume Paulo ao ya Ndugu Branham, linayo ruhusiya mtu kutafsiri ginsi anavyo taka. Mungu ndie mtafsiri wake mwenyewe na anakesha kwa Neno lake ili ayatimize yale aliyo ya ahidi. Taifa la Mungu lingeliweza kusimamisha kuamini matafsiri yanayo zunguka! Kanisa-bibi arusi inapashwa kurudishwa kwa hatua kamili, ililiweze kutembea katika umoja wa hatua ya kila Neno la Mungu! mbele ya kurudi kwa BWANA-Arusi, kwa kuwa wakati ni karibu saa ya maamzi imekuja.

## Swali La 1:
## Nimusimamo gani unayo kuhusu hudma ya Ndugu Branham?

**Jibu:** Nina amini mwito wa kimungu na Uteme wa Wiliam Branham, aliyo ilinganisha siku Juni, 11, 1933 ao kwa Mai, 7, 1946 ao kuhusu matukio nyingine za kimaajabu. Jambo la muhimu ambalo ni ujumbe aliyo ipewa Ndugu Branham kwa mwaka 1933, ilikuwa ya kutayarisha kuja kwa pili kwa Kristo. Tuna yaona yakitimia ulimwenguni katika myaka hii 40 inayopita mpaka leo. Katika mazowezi aliyo ipata siku ya Mai, 7, 1946, Ndugu Branham alipewa alama mbili za kimaajabu kama vile alizo zipewa nabii musa (Kutoka4:1-9). Ili aweze kukubalisha mkutano utume wake wa Kimungu wa hapo hapo! Wakati mgonjwa alipokuwa akiuona ugonjwa wake kwa mufano kansa na tumor na mengineyo, magonjwa yote yalikuwa yakionekana kwa mkono ya Ndugu Branham, ambayo yalikuwa ya kipotea wakati ya uponyaji. Mushuhuda wamzuri sana ambaye niliye kutana alikuwa Reverande Gordon Lindsay na Mke we Lindsay, Ambaye alie niambia kwa kipekee, ambayo aliye yiona ikifanyika kwa muda wa myaka tatu, ambawo walitembea pamoja na Ndugu Branham. Kwa alama ya pili ya kimaajabu iliyo julikana kama “Alama ya kimesia“ katika mwaka wa 50 na 60, ilishuhudiwa na ma million ya watu (Ona Baruwa ya Mzunguko, Spring 2005). Nami ni mushuhuda nilieona kwa sababu nilihuzuria mikutano ya Ndugu Branham katika Ulaya, na hata katika Marekani, na ni naweza kushuhudia Hudma hii ya kimaajabu mbele ya Mungu na wanadumu karama ya kinabii isiyoshindwa, ambayo Mungu alimupa mtu wa Mungu, ilipata ushuhuda wa kimungu. Kupitia hudma ya Ndugu Branham nafsi nyingi ziliongozwa kwa Kristo na maelfu ziliponywa na kufunguliwa sababu ya imani yao.

## Swali La 2:
## Ni toleo gani la haki alilo lipewa Ndugu Branham kwa Utume wake?

**Jibu**: „KAMA VILE YOHANA MBATIZAJI ALIVYO TUMWA MBELE KUTAYARISHA KUJA KWA KWANZA KWA KRISTO, UJUMBE ULIYO YIPEWA WEWE NDIYO ITAKAYO TAYARISHA KUJA KWA PILI KWA KRISTO“.

Musemo hiyo moja moja, Ndugu Branham ameisema zaidi ya mara 40 katika mahubiri tofauti. Kwa nini tena toleo hili liligeuzwa kwa

masemi ifwatayo: „Kama vile Yohana mbatizaji alivyo tumwa kutayarisha kuja kwa kwanza kwa Kristo, ndivyo hivyo nawe umetumwa kutayarisha kuja kwake kwa pili“. Maneno haya hata yalichapiwa kwenye mlango wa kuingia ndani ya nyumba mpya ya Ndugu Branham huko Tuksoni.

Ni mtu gani kwa duniani anaye ruhusiwa kubadilisha na kukataa utume halisi, ambayo ni; ujumbe utatangulia kuja kwa pili kwa Kristo? Mtu anaye fanya hivyo anamfanya ndugu Branham kuwa mwongo, kwa maneno aliyo yasema mara 41 akisema kwamba ujumbe ndiyo utakuwa mtangulizi wa kuja kwa Kristo. Na japo alitia mkozo akisema kuhusu utume wake,“ **Siyo kwamba mimi nita kuwa mtangulizi, baali Ujumbe ndio utakuwa mtangulizi“.** (Ushuhuda, Puetrorico, 2. 10. 1959). ni nani basi anaye sema ukweli? Ni wale watu wilio mjua Ndugu Branham kipekee, ao Ndugu Branham,mwenye unajuwa BWANA kwa kipekee?. Nikitu gani kinacho sukuma wandugu hao kuongoza watu wengine kwa uongo na kuwafunga katika kiroho kwa maoni yao? Wanaonyesha hudma iliyo pita wakiwaziya hudma itakayo kuja ya nabi, lakini kwa njiya hiyo wanapita kwa yale ambayo BWANA anayo yafanya kwa sasa.

## Swali La 3:
## Maoni yako nigani, Kuhusu Ujumbe ya Wakati wa Mwisho?

**Jibu**: Ni naamini na moyo wangu wote na nafsi yangu yote Neno la kweli la Mungu kama vile lilo tangazwa na William Branham kupitia neno „Ujumbe wa wakati wa wisho“. Kama vile kwa wakati wa mtume Yohana nami na weza pia kusema: *„Nihii ndiyo habari tuliyo isikia kwake, na kuyihubiri kwenu…“* (2. Yohana 1:5). Nina amini“Ujumbe wa wakati wa mwisho“ kulingana na neno liliandikwa la Mungu 100%. Ujumbe ni nene la Mungu halisi lililofunuliwa, pamoja na maahadi zote zilizo pewa kanisa la Yesu Kristo. Si amini tafsiri yoyote na teleo la uongo wanayoitilia kwa jina la“Ujumbe wa wakati wa mwisho“linalo onyeshwa na watu Fulani. Chochote kinacho toka kwa Mungu kinapatika tu katika mipaka ya neno la mungu. Na hailete matengano baali la ongeza bidii ya umoja wa waamini wa kweli katika miji na katika kila inchi na Duniani pote.

## Swali La 4:
## Jee, unamkosowa Nabii kwa mambo Fulani Fulani?

**Jibu:** Namna gani mtu anaweza fikiria kwamba mimi naweza kukosowa hudma ya kinabii isiyo shindwa! Wakati yoyote nina kuta maelezo ya kimafundisho tofauti kama vile, zaidi ya misemo makumi saba tofauti kuhusu ngurumo na maelezo mengi kuhusu masomo ya mahubiri kwa muda tofauti, sina majibu mengine isipo kuwa kurudi kwenye neno la Mungu. Kuna jibu moja tu kwa kilaswali la kibiblia. Maelezo tofauti inaonyesha ya kwamba jambo hilo lilikuwa bado kufunuliwa vema, na halinge weza kuwa kwanafasi yake kamili.

Tuna ona hudma kamili ya kinabii, iliyo shuhudiwa na maono, ndugu Branham aliona, na kama muhubiri, tunaona kwamba alikuwa na hudma ya Uinjilisti, na pia tunaona kwamba alikuwa akingojelea mambo makuu ambayo Mungu alikuwa anatarajia kufanya. Alikuwa tena nabii alieahidiwa kulingana na Malaki 4:5-6. Mwenye angepashwa kuja mbele ya kurudi kwa Yesu Kristo na kuweka kila kitu kwa nafasi yake kamili, kama vile BWANA mwenyewe alivyo ishuhudia katika Mathayo 17:11 na Marko 9:12. Alikuwa Yule ambae angeliweza kurudisha mioyo ya watoto wa Mungu kwa fundisho la kimusingi ya Wababa yaani Mitume, kwa kuwa kupitia hudma yake katika kanisa la Yesu Kristo mambo yote yange pashwa kurudishwa ili kanisa irudishwe katika utaratibu wa kimungu. Manabii walikuwa wamekwisha tangaza mambo yote mbele, lakini mitume na waalimu tu, wao ndio walikuwa wanapashwa kuyaweka kwa utaratibu katika mpango wa okovu wa Mungu. Tunapashwa kuheshimu maamzi ya Mungu kwa kuweka hudma tofauti kwaajili ya kukamilisha kanisa (Waefeso 4:7-16) na mengineyo). Mambo ambayo haikukuwa kwa nafasi sasa yaweza kuwekwa kwa nafasi yake kamili kwa namna ya mfano ya kimungu.

## Swali La 5:
## Yakini yako ni gani, Biblia ao Ujumbe?

**Jibu:** Swali gani hii! Yakini yangu ni sawa sawa na ya Ndugu Branham – Neno la Mungu, ambalo lina dumu milele. Hata Ndugu Branham alishimama mbele ya kusanyiko, akanyanyua Biblia yake na kusema, „*Hiindiyo yakini yangu!*“ kwa kweli swali hii haina maana: kwa kuwa maneno ya kweli yaliyo katika Ujumbe ni neno la Mungu lililo

funuliwa, ambamo munamo shauri zote za mpango wa okovu, kutoka mwanzo hadi mwisho wa nyakati na sana sana maahadi za wakati wetu. Na njoo maana Ujumbe ni Neno la Mungu na Neno la Mungu ni Ujumbe. Yeyote anaye weza kuyatofautisha yeye amedanganywa nay-eye ni inje ya utaratibu wa kimungu. Wahubiri wanao jiitilia ndugu Branham nakufundisha mambo mengine yasiyo lingana naneno la Mungu, wana mufanya kuwa nabii wa uongo, na tena wana zaraulisha Biblia. Ile kujidai kwao "Ufunuo" ime sambazwa kama Upumbafu.

## Swali La 6: Jee, Unafundisha Tofauti Nayale ambayo Ndugu Branham ali fundisha?

**Jibu:** Kuna watu wanao zaniya kwamba nina fundisha mambo mengi yaliyo tofauti nayale ambao nabii alifundisha, lakini vile nilivyo sema mbele kwa maelezo ya mwisho nilionyesha ya kwamba ukweli nikatika neno la Mungu. Ninayo mahubiri yote ya Ndugu Branham na nimeyaelewa, na kwasababu ya hiyo ninajua nimaelezo gani aliyo yaeleza kuhusu somo lile.

Kamavile kwa mufano, "Majuma za myaka" na sanasana kuhusu ma-juma"sabini za Danieli"wakati Ndugu Branham alisema kuhusu muda wawakati ya myaka saba na aliyo rudiliya kwa kusanyiko lote akise-ma, **"Juma moja ina linganishwa na myaka saba."** Alisema tena kuhusu myaka 3 kwa swali kama hilo nime sukumwa kuichunguza na maandiko ya Mungu ya hapo hapo. Wakati Ndugu Branham alipokuwa akilinganisha kwanyakati kati ya Unyakuo na utawala wa myaka Elfu, aliongea kuhusu myaka saba, nawakati alipokuwa akionyesha hudma ya manabii wawili wa lio ahidiwa kwa wayahudi, alisema kuhusu myaka 3. kama ni kuhusu fundisho, kurudilia maneno haitoshi, tuna pashwa yionyesha katika neno la unabii kwa mahali yake na nina wasihii, mufanye angalisho kwa nukuu ifwatayo: *"Wakati juma ya saba inaanza, myaka saba, kanisa limenyakuliwa. Mwaweza kuona hayo ndugu zangu? Inuweni mikono yenu juu ikiwa mwa weza kuona hayo … wakati juma ya saba inaanza, nikusema myaka saba, kanisa imenyakuliwa. Sasa sikilizeni, na waambieni na kuyarudiliya maratena, ili musiweze kuyasahau. Hii ndiyo Roho mtakatifu ameweka kwa kalamu yangu nilipokuwa niki andika…"*

Sasa tushike swali la 18 katika kitabu cha kingereza cha mihuri, Ukurasa wa 492, "Wakati a Agano la juma moja ya mwaka ya Danieli 9:27 itakapo timiya?" Jibu ni hii: *„Nusu ya agano hilo ilitimiya wakati yesu – Kristo alipokuwa duniani akiwa hubiri wa yahudi."* Hapo aliyarudiliya yale ambayo wengine waliokuwa wa mesema mbele yake. Kwahiyo wacha tuweze kupata maelezo bora katika Danieli 9:24-27, ambapo tunaambiliwa vema kuhusu Juma sabini za miaka ambazo zina sehemu tatu (3): nikusema 7+62+1. Hiyo ndiyo ASEMA BWANA katika maandiko kuhusu Kristo, Masiya kwa shahiri ya 26, *"Nabaada ya majuma sitini na mawili Masihi atakatiliwa mbali…"* Hili lilitimilika kwetu hapo Golgota. Baada ya hayo, katika sehemu ya pili ya shahiri la 26 tunasoma: *„…na watu wa mkuu atakaye kuja wata uangamiza mjii na patakatifu…"* Hiyo inasema kuhusu TITUS ambaye alikuja namajeshi ya Waroma na kubomowa muji na Hekalu kwa mwaka wa 70. Katika shahiri la 27 inaongeya kuhusu mpinga kristo, hapana Kristo, *"Naye atafanya agano thabiti na watu wengi kwa muda wa juma moja: na kwa nusu ya juma hiyo ataikomesha sadaka na dhabihu; na mahali pake litasimama chukizo la Uharibifu…"*

BWANA wetu alifanya Agano la milele pamoja nasi kupitiya Damu ya agano iliyo mwangika msalabani hapo karvari (Mathayo. 26:28, Marko. 14:24 na mengineyo). Kwamufano Yule anayeweza soma kitabu" Uongozi, Utaratibu, nayale 431 ya Maswali na majibu atakuta kwamba, Ndugu Branham alikuwa na misemo (maelezo mengi) katika mahubiri yake tofauti. Maandiko yana tuonyesha kwamba masihi atakatiliwa mbali (Danieli. 9:26) baada ya majuma sitini na mbili ambazo zilizo tanguliya majuma za myaka. Sehemu ya kwanza ya shahiri hii kama vile tulivyo waonyesha mbele, inaonyesha wazi wazi Yesu-kristo, masihi, na sehemu ya pili ina onyesha Mufalme wa kirumani. Danieli. 9:27; inaonyesha waziwazi kuhusu Mpinga kristo, pamoja na Agano la myaka saba ambayo itakuwa" Mapatano ya Kirumi" juu ya Yerusalemu. Kwa nusu ya juma la kwanza, manabii wawili watatimiza hudma zao (Ufunuo. 11); na kwa nusu ya pili ya juma baada ya agano kuvunjwa, Mpinga kristo anatawala myezi 42 ya Mauwaji na kuleta vita ya kupiganisha watakatifu (Ufunuo. 13:1-10). Na kwa hiyo wakati ya ziki ya Wayahudi, watajiachiliya kuuwawa, kwaajili ya utimilifu wa sehemu ya pili ya Muhuri wa tano (Ufunuo. 6:9-11). Hii ni kulingana na ASEMA BWANA katika neno lake takatifu.

## Swali La 7:
## Jee, Unaami kufunuliwa kwa Mihuri Saba?

**Jibu:** Ndiyo, Ninaamini kama mihuri saba ilifunuliwa kwa kimaajabu. Ndugu Branham aliniambia kwa kipeeke kwa mwanzo wa Disemba, 1962 kwamba yeye na jamaa yake wataenda huko Tucson kwa mwezi wa Januari 1963. Alikuwa ameabiliwa katika Ono, kwamba wakati utakapo fika wa kwenda huko Tucson, niwakati kazi ya upanuaji wa barabara uta kapo anza hapo mahali hapo uzio wake dongo utakapo bomolewa nakuangushwa chini na mashini za kutengeneza barabara zikizunguka barabarani. Kwamuda huo nilijioneya na macho yangu mwenyewe kazi hiyo kwenye barabara na uzio jinsi ulivyo angushwa chini kwenye udongo. Ndugu Branham alipewa Ono siku 22 Disemba 1962 kuhusu kuonekana kwa wingu kuu la kimaajabu, ambalo alikuwa amelizungumzia katika mahubiri yake ya siku 30 Disemba na suku 28 Februari 1963 alipo ambiwa kutoka katika wingu kuu la kimaajabu kuridi huko Jeffersonville, kwaajili ya kufunuliwa kwa Mihuri.

## Swali La 8:
## Jee, Na Muhuri wa Saba Umefunuliwa?

**Jibu:** Yeye anaye soma ao kusikiya mahubiri kuhusu mihuri saba, atakuta kwamba kila wakati Ndugu Branham alisoma Ufunuo maneno yote ya kila muhuri, tukitosha muhuri wa saba. Hapo alisoma tu ukurasa wakwanza wa sura 8, ambayo ina sema kuhusu kimya katika mbingu muda wa nusu saa. Aliifunga hii muhuri wa saba na mambo mengi tofauti. Na akaongeya kuhusu mwisho wa nyakati za kanisa, na mwisho wa baragumu, na mwisho wa hivyo vikombe vya hasira ya Mungu, ndiyo kusema mwisho wa mambo hayo yote. Mtu anaye soma maneno ya Ufunuo 8 kuanzia ku shahiri ya 2, atasikiya kunasemeka wa malaika saba wanao jitayarisha kupiga baragumu hizo saba.

Kuna malaika saba wa ma kanisa saba (Ufunuo sura 1 mpaka 3).

Tena, kuna wa malaika saba wenye Baragumu (Ufunuo sura 8 mpaka 11).

Na kuna wa malaika saba wenye vikombe vya hasira ya Mungu (Ufunuo 15 na 16). Wote wako na nafasi yao katika utaratibu ya kiungu.

Nukuu: „Katika sehemu tatu za kwanza za Ufunuo, mambo yote ya nayo husika na kanisa yame funuliwa. Baada ya hayo, hatuoni kitu yengine kuhusu kanisa hadi sura ya 19. Kwa sura ya 4, kanisa inanyakuliwa na inarudi tena kwa sura ya 19. BWANA arusi na Bibi arusi wanarudi pamoja duniani. Kwa sura ya 19 na 22 munamo mambo yote yanayo husu myaka Elfu na yenye itakuja baadae. kati ya sura ya 4 na 19, mungu anahusika na Israeli" (Sikukuu ya baragumu sura ya 5 na 30). Ndugu Branham aliweka mkazo maranyingi. Nina wasihi wacha hili liandikwe katika herufi kubwa: *„SURA YA 4 NA 19, MUNA FUNGIWA NDANI SURA YA 8 NA 9, 10 NA 11"*. Katika sura hizi inne zote, hamuna kitu chochote kinacho husu Kanisa kama vile Ndugu Branham alivyo sema mara nyingi.

Kulingana na muhuri ya saba, kiti cha neema kitaka pogeuka kiti cha hukumu, hapo hakutakuwa mupatanishi tena wa kupokeya maombi ya watakatifu (Ufunuo. 8:2-5). Hapo sasa moto kutoka kwenye madhabahu utatupwa duniani. Ndipo kuta fuata sauti za Ngurumo na Umeme na mengineyo.(Shahiri la 5) Ndugu Branham aliambiwa ya kwamba baragumu saba hazihusike na wakati wa nyakati za kanisa.

Nukuu: „…Hapohapo baada ya wamalaika wa BWANA walipo onekana kwangu na kuniambiya kuhusu baragumu saba ao mihuri saba …hapo ndipo Roho-mtakatifu alinionyesha kwamba hazina mafaa yoyote kuhusu kanisa kwa wakati huu, sababu haikukuwa namaana kwa kanisa…baragumu zinakazi kwa kukusanya wa Israeli …Kumbukeni hayo, kila baragumu ina sikilikana wakati wa muhuri wa sita…ninamna gani ilivyo kamili baragumu ya saba na muhuri wa saba!" (Siku kuu ya baragumu, 19 Julai, 1964)

## Swali La 9:
## Jee, Unaamini Kwamba Ufunuo 10:1-7 Imekwisha timiya?

**Jibu:** Ufunuo 10 haija timiya bado. Kama vile tume kwisha kuiona, hiyo haina uhusiano na kanisa. Ngisi inavyo andikwa ndani ya Ufunuo.3:14-22 Ndugu Branham alikuwa mjumbe wa kizazi chamwisho cha kanisa na si malaika wa baragumu. Alikuwa akijilinganisha na Ufunuo 10, kwa sababu nimahali moja tu katika Biblia ambapo kuna semeka kuhusu Ngurumo saba. Kwa hiyo tunatambua hali za nyakati hizi mbili tofauti katika Unabii. Kama kwa mufano Matayo. 2:15 inaonyesha utimilifu wa neno lililo katika hoseya. 11:1."Nime muita mwana wangu toka misri"ili litimiye kwa ajili ya Yesu-kristo, na yale yaliyo andikwa katika Kutoka. 4:22 yana dumu bila kubadilika: *„Bwana ase-*

*ma hivi, Israeli ni mwanawangu, nami nimekuambia… Mpe mwanangu ruhusa aende, ili apate kunitumikia…“.* kuna unabii wa kibiblia ambao una weza tumikishwa mara mbili. Lakini hata ingawa inaweza kuwa vile, ni lazima iachwe kwa nafasi yake kamili ampapo unastahili, kulingana na mupango wa okuvu. Utimilifu wa kweli wa Ufunuo 10 ulitangazwa mbele na utaeleweka zaidi kupitia maandiko yataka yo fuata. Mara tena tunaoneshwa lazima ya kiungu, ya kwamba kilakitu kinapashwa jengwa kupitia zaidi ya andiko moja.

Neno la kwanza la Muhimu **“kuunguruma“**

*“Ata unguruma kwa sauti kubwa kama vile simba anguru mavyo“* (Ufunuo 10:3)

*“…BWANA atanguruma toka juu, naye atatoa sauti yake toka patakatifu pake, atanguruma sana juu ya zizi lake…“* (Yeremia. 25:30)

*“Wata kwenda kumufuata BWANA, atakae nguruma kama simba; kwa maana atanguruma, nao watoto watakuja kutoka mangaribi…“* (Hosea 11:10)

*“Nae BWANA atanguruma toka sayuni, atatoa sauti yake toka Yerusalemu; na mbigu na nchi zitatetemeka; lakini BWANA atakuwa kimbilo la watu wake, na ngome ya wana wa Israeli“* (Yoeli 3:16).

*“…BWANA atanguruma toka sayuri, atatoa sauti yake toka Yerusalemu…“* (Amosi 1:2)

Neno la kufata la muhimu “**kuapa“**

*“Na Yule malaika nilie mwona, akisimama juu ya bahari na juu ya nchi, akainua mkono wake wa kuume kuelekea mbinguni, akaapa kwa yeye alie hai hata milele na milele, yeye alie ziumba mbingu na vitu vilivyomo, na bahari na vitu vilivyomo, ya kwamba hapatakuwa na wakati baada ya haya…“* (Ufunuo 10:5-6)

*“Nami nika msikia Yule mtu alie vikwa nguo za kitani aliekuwa juu ya maji ya mto, hapo alipo inuwa mkono wake wa kuume na mkono wake wa kushoto kwelekea mbinguni; akaapa kwa yeye alie hai milele na milele, ya kwamba itakuwa wakati…“* (Danieli. 12:7) Hii haingeliweza kusemwatena waziwazi kwamba tangu muda huo alipo apa, kunabaki tena myaka mitatu na nusu mpaka wakati wa mwisho. Kwa uhakika nyakati hizi ziko kwa nafasi yake kamili!

Wakati BWANA anashuka kama malaika wa Agano, ataweka muguu yake kwa bahari na nyingine kwa udongo, na kusamba mamlaka yake mwenyewe! Hapo ndipo ngurumo saba zitatoa sauti yazo. Tunapashwa jua kwamba kila andiko linapashwa pata utimilifu wake katika maandiko na kila tafsiri ni udanganyifu wa mwovu. Vile ndivyo vilivyo hata kwa sehemu ya pili ya Malaki 3:1-2, yenye ilikuwa bado kutimilika kwa wakati wa kuja kwa kwanza kwa Kristo. Nandio maana haikusemeka katika Agano Jipya, lakini wakati ile kitendo kitatendeka ndipo litatimia *"...Naye BWANNA mnae mutafuta atalijia hekalu lake gafla; naam, Yule mjumbe wa Agano mufurahiae, angalieni, anakuja, asema BWANA wa majeshi. Lakini ni nani atakae stahimili siku ya kuja kwake? ao ninani atakae simama atakapo onekana nayeye? kwamaana yeye ni mufano wa moto wa mtu asifishae fedha..."* (Malaki 3:1-2). Hii kuja kama malaika wa Agano, ambayo imesemeka kwa urefu; kwa maandiko ambazo zimesomwa hapo nyuma inastahili kuwekwa mahali ambapo maandiko inaiweka – pamoja na Israeli. Kwa wakati huo hekalu litakuwa lime kwisha kupimwa na kujengwa tena kulingana na Ufunuo 11:1-2, Hapo sasa ndipo huyo malaika wa Agano ambae ni BWANA wa majeshi, ataingia. Amina!

## Swali La 10:
## Jee, unaamini ya kwamba ngurumo saba zimefunuliwa kwa ndugu Branham?

**Jibu:** hapa kuna maneno ambayo ndugu Branham aliyo ya sema kuhusu somo hilo katika mahubiri yake ya mwisho ya siku, 15 Ogusti 1965, **"...ngojeeni mpaka tutakapofikia kufunuliwa kwa mapigo, mihuri, na ngurumo saba."** Aliongeya kuhusu ngurumo saba zaidi sana akiambatanisha na hiyo tukiyo kubwa lililofanyika siku 28 Februari 1963, wakati alipo sikia sauti ya ngurumo saba zenye nguvu na wingu kubwa lakimaajabu lika onekana. Dr JAMES MC DONALD, wa univasta ya Tukso, alilinganisha Picha nyingine zilizo kamatwa, hapo ndipo wapasha habari wa *"Science"* magazine siku 19 Aprili 1963 na *"Life"* magazine siku 17 May 1963 ndio walio tangaza tukio hilo. Nayale yanayo semeka kuhusu hilo. Kufwatana natukio hili Ndugu Branham aliongeya kuhusu imani ya unyakuo, jina mpya ambalo litafunuliwa naaliambatanisha na matukio mengine ya muhimu.

Ngurumo saba za Ufunuo zinastahili kuachwa mahali zilipangiwa na Mungu. Sababu zitatoa sauti yazo wakati Malaika wa agano anashuka kwa Israeli (kitabu cha mihuri saba Pg 72). Mafundisho yanayo sema kwamba ngurumo saba ni“ nguvu saba“ao“watu saba wa ajabu“ ao matafsiri yoyote kuhusu ngurumo, zina stahili kukataliwa mbali, kwa sababu nima tasfiri ya watu binafsi, na masemi ya watu ambayo hayana msingi wa kibiblia (wa kimaandiko).

Baada ya Ndugu Branham kuhubiri mihuri saba, aliambiwa kurudi kwa maskani yake na kusema mambo Fulani ya muhimu, kati yahayo munamo maelezo yafwatayo: „Kama hivi, inavyo andikwa kwamba hakuna mtu aijuae saa ya kuja kwake; na hivyo ndivyo hakuna mtu anae jua siri za ngurumo saba“ (Kitabu cha mihuri saba Pg 576)

Wahubiri, mtoe mikono yenu kuhusu ngurumo saba, na mkaiachiye Mungu mwenyewe. Yohane hakuruhusiwa kuandika yale ambayo ngurumo saba zilisema. Namaneno hayo hayakupata nafasi katika neno lillilo andikwa la Mungu, na kwasababu hiyo haiwezi kuhubiriwa: Hii ni ASEMA BWANA katika neno lake, tume amuriwa kuchunga mambo ambayo yanaandikwa pekee. (Ufunuo. 1:1-3) natume katazwa kuongeza jambo lolote kwa kwamaneno ya unabii wa kitabu hiki. (Ufunuo. 22:16-21) Kweli hii sini arifa iliyo wazi?

## Swali La 11:
## Kwa nini Ndugu Branham
## aliongeya mara nyingi kuhusu “Mvuto Wa tatu?“

**Jibu:** Musemo “mvuto wa tatu“ ina maanisha sehemu ya tatu naya mwisho ya hudma yake. Nukuu: „MVUTO WA KWANZA-kuponya, MVUTO WA PILI-Kutabiri. MVUTO WA TATU, KUFUNULIWAA KWANENO, MASIRI ZIKAFUNULIWA…“ (Vitu vya dhahabu Pg 158). Siku 28 Februari 1963, Ndugu Branham alisikiya sauti za ngurumo saba zenye nguvu alizo ziita kila wakati “Ngurumo saba“ kwa kweli alipiga kwenye madhabau mara saba na ngumi yake, akisema: “Sauti za ngurumo saba, zili fwatana moja baada ya nyingine zilikuwa zenye nguvu, zilikuwa zinataka onyesha kitu Fulani.“ (Muhuri wa saba, siku 24 machi 1963). Tena aliongeya kuhusu siri ambayo shetani hajuwi na pia kuhusu “Mvuto wa tatu“ – kuhubiri wale waliyo potea. Alisema tena kuhusu upanga wa mufalme ulio wekwa mikononi mwake na akaweka musemo mara tena “Hii ni mvuto wa tatu“ Alisema tena kuhusu hudma ya neno lililo nenwa.

Jambo lamuhimu nikwamba tuna pashwa pambanuwa tofauti gani iliyo katika ngurumo saba zilizo sikilikana wazi wazi alipokuwa kwenye mlima sunset, mbele ya kuvunjwa kwa mihuri saba na ngurumo saba za Ufunuo 10 ambazo zitatowa sauti yake wakati Malaika wa Agano atakapo shuka akishika kitabu chenye kufunguliwa katika mkono wake. Sauti ya Mungu inasikilikanaka kama vile sauti ya ngurumo yenye nguvu! *“Zisikilizeni hizo kelele za sauti yake, na uvumi utokao kinywani mwake … Mungu huunguruma kwa kustaabisha kwa sauti yake, hufanya mambo makuu ambayo hatuwezi kuelewa nayo“* (Ayubu 37:25). Tuone tena kutoka 20:18, Yohana 12:28-29, Waebrania 12:18-19 na mengine).

## Swali La 12:<br>Kwa nini ndugu Braham<br>maranyingi alijilinganisha na Ufunuo 10:7?

**Jibu:** Nimushangao kuona karibu nusu ya maswali yote yana ulizwa kwa namna moja yakieleza kwa Ufunuo 10. Twaweza fanya angalisho tena kwa yale ambayo yalisemeka: Alipokuwa akiongea ku Ufunuo 10:7, alirudilia akisema kwa uwingi kuhusu “Masiri“, haiko kuhusu “siri moja“, ambayo ni “siri ya Mungu“. Ndugu Branham alifanya hayo, kwa kuwa yeye ndie aliekuwa mjumbe wa kanisa la kizazi cha saba, ambamo siri zote zilizo fichwa kupitia yeye. Katika mahubiri yake: „Je mabwana hii ndiyo wakati?“ ya siku 30 Disemba 1962, ndugu Branham alitoa masiri kumi na saba tofauti ambayo zilizo funuliwa. Alianzana na“siri ya Ufalme wa Mungu“na anamaliza na“siri ya kurudi kwa nguzo ya moto“. <u>Yesu kristo ndiye Siri ya Mungu.</u> Hii tunaikuta ikishuhudiwa na 1. Timotheo 3:16 ambapo tunasoma kuhusu“siri ya Mungu“ni katika musemo ya umoja. Wayuda hawa kukubali ufunuo na kuonekana kwa Mungu moja wa kweli katika Yesu Kristo, na mpaka sasa hawaja litambua. Ila kanisa la Agano Jipya lilijua siri ya Mungu toka mwanzo (Wakolosai. 2:2-3, na mengine yo).

Kwa wakati tukiyo hili la ajabu “Siri ya Mungu“ linafikia mwisho, wayuda wataingizwa, kamavile ilivyo funuliwa kwa watumwa wake, manabii. Wakati kanisa la agano Jipya linaonyeshwa, tunasoma neno <u>Mitume na Manabii</u> kwa sababu kanisa la Yesu Kristo limejengwa kwa musingi wa mitume na manabii (Waefeso. 2:20). Wakati kitu kina semeka kuhusu Wayuda, yenye inasikilikana ni *„…kama vile alivyo wa-*

*funulia watumishi wake manabii*" (Amosi 3:7). Baada ya matangazo katika Ufunuo 10:7, Yohana angeli kula kitabu kinacho funguliwa na aliagizwa: *„Unastahili tabiri mara tena…"* Kwa sura 11, manabii wawili wa Israeli watatabiri muda wa myezi 42 huko Yerusalemu, inayo lingana na miaka mitatu na nasu. sihiyo yiko wazi wazi?

Kwa sura ya 8 na 9, ndimo tunapo kutana baragumu sita za kwanza za hukumu na kwa sura ya 10 kunapatikana taganzo.Utimilifu wa kweli wa hio iko kwa sura ya 11, mustari wake 15: *„Malaika wa saba akapiga baragumu, pakawa na sauti kuu katika mbingu, zikisema ufulme wa dunia umekwisha kuwa ufalme wa BWANA wetu na Kristo wake, naye atamiliki hata milele na milele."*

Tunastahili kuheshimu utaratibu wa Kiungu unayo oneshwa kwetu katika neno la Mungu. Baada ya baragumu ya saba kulia hapo tuna soma: „…kasirani ambao itakuja, na wakati ya hukumu kwa wale waliokufa…kama vile *"…kuwapa malipo watumwa wake, manabii, na watakatifu…"* (Ufunuo.11:15-19). Niya muhimu sana kujua kwamba neno la kihebrania "Shofar" imetafsirssiwa katika biblia zetu kama"Baragumu", kulingana na muhuri wa saba na malaika saba wenye baragumu, tangu sura ya 8:2 na kupitia sura 9, na sura ya 10:7 mpaka sura ya 11:15, hii neno "Shofar" imetumikishwa mara 11. Hizi "Shofar" (baragumu) tatu za mwisho, zina tangazwa kama vile "sauti", zinapatikana katika Ufunuo 8:12 na pia katika Ufunuo 10:7*: „Ole, ole wao wakaao juu ya nchi!kwa sababubu ya sauti zisaliazo za baragumu za malaika watatu, walio tayari kupiga baragumu!"* (Ufunuo 8:13).

*"…isipokuwa katika siku za sauti ya malaika wa saba atakapo kuwa tayari kupiga baragumu…"* (Ufunuo 10:7)

## Swali La 13:
## Jee, Unaamini Hudma ya Mjumbe wa mnane?

**Jibu**: APANA, siamini mtu yeyote anaye jiita mjumbe wa munane ao kuamini yale anayo ya sema. Kulingana na Ufunuo 1:20 kuna nyota saba tu – Malaika saba wa vizazi saba vya Kanisa katika mkono wa kuume wa BWANA aliefufuka.

Nikusema ikiwa kuna Malaika yeyote wa munane ana weza patikana kwa mkono wa mwengine, kwa kuwa kuhusu huyu hakuna ahadi yake katika maandiko matakatifu. Haiseme hata Yosua, Elisa ao Nabii

mkubwa atakaye kuja kwa ajili ya Kanisa. Kila mutumishi wa kweli wa Mungu kwa wakati huu anasimama kwa msingi mmoja moja na anatangaza Neno la kweli-Ujumbe wa wakati unao tangulia kuja kwa pili kwa Kristo.

## Swali La 14:
## Unaamini fundisho la Parousia?

**Jibu**: Kwa swali hii ni jibu moja moja ninalo toa. Wakati BWANA anakuja, nitachukuliwa katika utukufu pamoja na watakatifu wote. Kila kuja kwa BWANA ni uhakika na ataoneka katika mwili. Neno hili "parusia" inamanisha kuja kwake katika mwili. Wakati wowote Bibi-Arusi akingali duniani, nikusema BWANA-Arusi bado hajakuja. Wakati atakuja kama BWANA arusi, wafu waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza, nasi tulio hai tuta badilishwa pamoja tutaenda kumulaki BWANA katika mawingu (1. Wathesalonike 4:13-18). Kwa uhaki hakuna ahadi katika neno la Mungu linalo sema kwamba Kristo ataanza kuja duniani amalize muda kidogo pamoja nasi mbele ya unyakuo kufanyike. Kwa kweli tume arifiwa: „*Wakati huo mtu akiwaambia tazama, Kristo yupo hapa ao yuko kule msisadiki*" (Mathayo 24:23). Akawajibu: „*Kwa maana kama vile umeme utakavyo mashariki ukaonekana hata magharibi, hivyo ndivyo kutakavyo kuwa kuja kwa mwana wa Adamu*" (Mathayo 24:27). Hakuna tena ahadi ya kwamba kushuka kwake kutaanza wakati wa kufunuliwa kwa mihuri ao kwamba kiti cha rehema kitabadilishwa kuwa kiti cha hukumu kwa wakati ule.

Mafundisho ambayo si ya kimaandiko inatokana na kuelewa vibaya maandiko na matafsiri ya watu binafsi. Ndugu Branham alikuwa akisema: „Kwanza ni ujumbe inayo tangulia, mkate uliyo hai wa uzima. Kupitia yeye bibi arusi emeitwa kutoka…Ni jumbe inayo ita taifa kukusanyika, kwanza Ujumbe unatangulia, sasa ni wakati wa kusafisha mataa, Amkeni mukasafishe taa zenu. Ilikuwa kwa saa gani za usiku? Ni kwa saa ya saba ! apana ya sita, kwa saa ya saba. Tazama BWANA arusi tokeni mwende muka mlaki, Amkeni mukatengeze taa zenu!" Tazama namna gani Roho mtakatifu anavyo ongoza toka 1. Wathesalonike 4 hadi matayo 25 mahali tunasoma kuhusu kelele ya usiku wa manane. Ni mwito wa kuamsha mabikira kumi ambao wote walikuwa katika usingizi. Kulingana na shahili la 10, wale wote ambao wata kuwa tayari wakati BWANA arusi

atakuja wataingia pamoja naye katika chumba ya arusi. Twaweza soma katika Ufunuo 19:1-10 ile ambao inahusu karamu la arusi, yeyote anae tofautisha arusi na karamu anapashwa soma Mathayo 22, ambapo arusi na karamu vinatumikishwa mara saba, kama vile kitendo kimoja. Arusi na karamu vitatendeka huko mbinguni (Ufunuo. 19:1-10), siyo duniani. Kanisa Bibi-arusi toka katika vizazi vyote wataonekana katika arusi pamoja na Abrahamu, Isaka, Yakobo na pamoja na wale wote waliokombolewa.

### Swali La 15:
### Jee, unaamini kwamba mwana wa Adamu amekwisha kuja kulingana na Luka 21:27?

**Jibu:** La, Sivyo. Kwa kweli mimi siamini yakwamba mwana wa Adamu amekwisha kuja. Ninaamini ya kwamba mwana wa Adamu alijifunua ye mwenyewe kwa njia hiyo moja na kwa alama hiyo moja ya mesiya kupitia hudma ya kinabii, kama vile alivyo fanya ndani ya Yesu alipokuwa akitembea duniani (Luka 17:30). Kwa sura ya kwanza ya Yoane, Natanaeli na Simoni Petro waliishi mazoezi hayo; kwa sura ya 4 ya yoane, pamoja na Yule mwamke kwenye kisima chamaji, katika mat 21 pamoja na wanafunzi wake, wa lio leta punda na mwana punda kwake, ili neno la Zekaria 9:9 liweze kutimia. Kuja kunako semeka katika Luka 21:27, haina uhusiano pamoja na kurudi kwa BWANA-Arusi akija kuchukuwa Bibi-arusi mbele ya ziki kubwa: Hiyo kuja kwa mwana wa Adamu kutafanyika baada ya ziki.

*"Lakini mara, baada ya dhiki ya siku zile, jua lita tiwa giza, na mwezi hautatoa mwanga wake … Ndipo itakapo onekana ishara yake mwana wa Adamu mbinguni; ndipo mataifa yote ya ulimwengu watakapo omboleza, nao wata mwana wa Adamu akija juu ya mawingu ya mbinguni pamoja na ngavu na utukufu mwingi"* (Mathayo 24:29-30, Marko 13:24-32, Luka 21:25-33). Jambo hili ni wazi kwamba baado halija fanyika. Hii kuja yaweza kulinganishwa tena na Daniele 7:13, na Ufunuo 1:7,*"Tazama, yu aja na mawingu; na hao walio mchoma; watamwona; na kabila zote za dunia wataombo leza kwa ajili yake. Naam Amina"*. Kitendo hiki cha kuja kina husu mataifa yote na zaida sana wa yahudi, ambao hapo ndipo watamtazama Yule ambayo walio mchoma (Zekaria 12:10).

**Swali La 16:**
**Ninamna gani na hudma yako? Inapatikana katika Biblia?**

**Jibu**: Utume ambao BWANA amenipa isingekuwa katika maandiko matakatifu singe kuwa na ruhusa ya kuitwa mtumishi wa Mungu. *“Na Mungu ameweka wengine katika Kanisa: wakwanza Mitume, wa pili manabii, watatu Waalimu…“* (1. Wakorintho 12:28). Ndugu Branham alisema; “Hakuna mtu anae ruhusa ya kuhubiri, kama haja kutana na Mungu, kama vile Musa alivyo kutana na Mungu mwenyewe…“ (Kitabu, Makao yatakao kuja). Kila mutu alie itwa na Mungu anajua siku, na saa, na Mahali na maneno aliyo yapewa kuhusu utume wake. Ushuhuda wangu unajulikana ulimwenguni pote, kwa muda wa myaka mingi. Ilitangazwa huko Ujerumani na wapasha habari wa “Voice of Healing“yaani“ sauti ya uponyaji“kwa mwezi wa Machi, 1963 washuhuda wa wili, Fred Sothman na Banks Woods, walikuwa mahali pale siku ya 3, Disemba, 1962, wakati ndugu Branham kupitia Ufunuo wa kiungu, alirudilia Neno kwa neno kwa yale ambao Mungu alikuwa aliniambia siku ya 2, Aprili, 1962. Sijawai kusahau namna nabii alisema: „Ndugu Frank, Ulielewa vibaya yale ambayo BWANA alikuambia. Ulizani kwamba hapo kutakuwa njaa ya Mwili na wewe ukaweka chakula cha mwili“ Aliendelea akisema“ BWANA atatuma njaa ya kusikia maneno yake. Chakula ambacho unastahili kuweka ni Neno lililo ahidiwa la wakati huu… linapatikana katika mahubiri yalio shikwa kwenye Kanda… kwa hiyo subiri kwa ugawaji mpaka utakapo pokea mabaki yake“. Utume ambao niliupewa una sehemu mbili kwanza, kwenda katika mji, toka kwenda katika miji nyingine kwa kuhubiri Neno, Ya pili: kugawa chakula cha kiroho.

Kupitiya njiya ya Mungu ilikujatimiya wakati Ndugu Don Bablitz alipo kuja kuniona wakati nilipo kuwa huko Edmonton katika nyumba ya wittmeir inayo patikana mahali ya 137 kwa Ogusti, 1976. Ndiye aliyekuwa pamoja na kundi, kwa myaka mingi wakituma mahubiri ya Ndugu Branham kwa anuwani zote. Nami nilikuwa nikipokeya wakati nilipo kuwa nikitembeleya inchi tofauti, kwa hiyo a subuhi ya juma mosi alisema akiniambia“Ndugu Frank, tuna ona hudma ya Ndugu Branham katika Biblia, Namna gani kuhusu hudma yako? Nayo inapatikana katika Biblia? Nilimugeukia ni kisema: „Na kusihi, simamiya hapo. Usiseme hilo. Namna gani hudma yangu yaweza kuwa katika Biblia?…“

Unaweza ukaamini ao usiamini, Lakini asubuhi ifwatayo niliamka mapema, Nika vaa, nika kaa kwenye pembe la kitanda na nika sogea kushika Biblia yangu, kwa mukono wa kuliya ka ma vile inavyo tendeka kwa kila mara BWANA akasema maneno haya kwanguvu nasauti kubwa yenyenguvu na mamlaka"MTUMISHI WANGU NIMEKUWEKA KWAKUGAWA CHAKULA KULINGANA MATHAYO 24:45-47". Nilikuwa bado sijajuwa maandiko haya katika Biblia ya ugawaji wa chakula chakiroho cha wakati huu. Mungu alikuwa amesema kwamba atatuma njaa ya kusikiya neno la BWANA (Amosi 8:11). Hii ndiyo sababu Ndugu Branham aliambiliwa kuweka Chakula chaKiroho, Ambacho kinagabuliwa kwa wakati huu. Hudma ambao Mungu amenipa hapo hapo ina ambatana na hudma ya Ndugu Branham. Ni jambo moja ya kuweka chakula kwa uwingi, kama vile Ndugu Branham alivyo onyeshwa, na jambo lingine ni kuwekea taifa la Mungu chakula chakiroho tayari kwenye meza ya BWANA.

Wa ndugu wote walio pokea mwito wa kiungu duniani pote kutumika katika nyumba ya Mungu wana dumu katika Neno na wana sehemu kwa ugawaji wachakula cha kiroho.

## Swali La 17:
## Jee, Unahubiri mahubiri ya Ndugu Branham?

**Jibu:** La, sihuburi mahubiri ya Ndugu Branham, kwa kuwa imekwisha tayari kuhubiriwa. Nina yatafsiri, na kuya tangaza. Na ndivyohivyo kwa wale ambao wanayo yihitaji wanaweza kulisha nafsi zao wanapo ya sikia ao wanapo yasoma. Nina hubiri tu Biblia, Lakini yawezakana, kufwatana na uongozi wa Roho Mtakatifu nina weza pia kutumia maneno (ma Nukuu) kutoka katika mahubiri yake.

## Swali La 18:
## Chakula chakiroho ni gani, jee ni mahubiri ya Ndugu Branham ao Biblia?

**Jibu:** Ninani angeliweza uliza swali kama hili? Itabaki kuwa kweli milele kwamba mtu wa kiroho hataishi kwa mkate tu wakimwili bali kwa mkate utokayo mbinguni (Yohana 6:32-59). Chakula cha kiroho ni Neno la Mungu linalo tuweka nguvu kufanya mapenzi ya Mungu

(Yohana 4:34). Tunapo soma Biblia nakuipokea kupitiya mahubiri, kwa wateule wanao amini neno itatimiza kile ambacho lilitumwa kufanya. Katika mahubiri ya Ndugu Branham tunakuta neno lililo funuliwa na Mana iliyofichwa ya moto kwa wateule. Hii ndiyo lengo la kiungu ambalo linaambatana na sehemu ya hudma ya Kinabii na Kufundisha.

## Swali La 19:
## Ninani atakaye lionyesha kanisa la wakati wa mwisho kwa BWANA?

**Jibu:** Ilikuwa itaji ya mtume Paulo la kumulika kwa Kristo Kanisa lililo safi kwa wakati wake (2. Wakorintho. 11:2-4). Lakini, mtume alikuwa akiogopa kuwa kama vile Hawa alivyo daganywa na nyoka, mafikiri ya waamini isidaganywe na kutoka kwa unyenyekevu kwa Kristo. Pia anaonyesha namna upotevu ulivyo ingizwa: kupitia wale wanao hubiri Yesu mwengine, na wakitangaza injili ingine sababu walipokea roho nyingine. Kulingana na Waefeso 5:26-27, BWANA Yesu mwenyewe, atajiletea Kanisa lake mbele yake*: „Apate kujiletea Kanisa tukufu, lisilo na hila wala kunyanzi wala lolote kama hilo; bali liwe takatifu lisilo na lawama“*. Mtu wa Mungu anahubiri tu Neno, Lakini BWANA mwenyewe ndie Neno, alikomboa kanisa lake, ana waita waliyo wake kutoka na ndiye mwenyewe atakae timiza kazi yake ya ukombozi. Wale walio hubiri wata kuhukumiwa mbele ya macho ya wale ambao waliwahubiri. Kulingana na yale ndugu Branham aliona alipo chukuliwa nyuma ya ukuta wa nyakati. Hii inatembea na maandiko katika Warumi 14:7-12, na 2. Wakorintho 5:9-10 mahali Paulo anasema: „Kwa maana imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo“.

## Swali La 20:
## Unajisikia jee, kwa wale wanao zihaki jina lako?

**Jibu:** Mimi sijisikie vibaya, ila tu hiyo ina nisukuma kuwabariki wale ambao hawawezi kuchunga chuki yao: Nahiyo haifanyiki kwangu peke yake, ila ni kwakila mutumishi wote wa Mungu anaye tangaza neno la Mungu kama vile mtume Paulo alivyo sema*: „Kwa utukufu na aibu, kwakusemwa vibaya na nakusemwa*

*vizuri, kamawadanganyifu; bali tu watu wa kweli"* (2. Wakorintho. 6:8). wakati nyingine kwamfano mambo yasiyoyakweli na mazihaki yanasambazwa, kupitiya baruwa zilizo wazi, hata kwenye madhabau, na kwamtandao, hata nakatika vitabu vyao vinavyo eleza kuhusu ngurumo saba. Hivi tunatambua kama hizi ndizo mbinu ambazo shetani anatumiya ili apate namna ya kubomoa ushawishi wa utume wa kimungu. Hapo natambuwa kama shetani anatumikisha watu hao. Hivyo ndivyo alivyo fanya kwa watumishi wote wa Mungu. BWANA yesu aliye niita hunipa nguvu mupya kilasiku ili niweze kugawa neno la kweli la Mungu pamoja na waamini wote wa kweli. Ingawa matusi yote ninayo yavumilia, ninaweza tu kuwatakia mema kwa wale maadui wakale na wa sasa wanao kataa kweli. Niwale viongozi wa kidini walio saliti manabii na kuzihaki BWANA na mitume kwakuwa walikuwa vipofu katika roho na walitaka waongoze vipofu. Tabia ya mbegu ya kweli itajionyesha yenyewe. Hauwezi chuma tini kwenye miiba, nakwa chemuchemu moja hakuwezi toka maji matamu na maji machungu. Wengi wanapenda kwa namna ya kaini (1.Yohana 3:11-12), ambao ilizaa mauti wakati ule; kwaleo sasa kuna mauwaji ya kitabiya. Kaini na wivu yake, na Abeli aliye kubaliwa na BWANA, ni mfano mbele ya macho yetu. Uadui na wivu, vyazaa mauti.

Nukuu: *„silazima kutumia upanga kumchoma mwenziyo mgongoni kwa kumuuwa. Unaweza kubomowa ushawishi wake na kuuwa ushawishi wake. Kusema vibaya mchungaji wako, ukisema mambo mabaya juu yake: Nikama vile kumchoma upanga. Kusema kitu chochote kisicho chakweli kwa mutu, hiyo itabomowa ushawishi wake mbele ya watu, na*

*utahukumiwa!Hivyo ndivyo alivyo sema yesu"* (vitu vya zahabu Pg. 167).

Isaka na Ishimaeli walikuwa watoto wa baba moja: kwa hivi yule aliyezaliwa kwa mwili alimchukia yule aliye zaliwa kwaahadi. Basi ndugu zangu kama isaka sisi niwatoto waahadi. lakini kama vile siku zile aliye zaliwa kwa mwili alivyo muudhi yule aliye zaliwa kwaroho, ndivyo ilivyo na sasa (Wagalatia. 4:28-30). Hiyo haiwezi kubadilika. Hiyo haiwezi kufichwa."kila amchukiaye ndugu yake nimuuwaji: Nanyi munajuwa yakwamba kila muuwaji hana uzima wa milele ukikaa ndani yake." (1.Yoane 3:15). Hii nikweli yakujaa. Yeyote amchukiae ndugu yake na ku muuwa kwa maneno mabaya kwakweli „anajiuwa mwenyewe"kwasababu anapoteza uzima wa milele.

## Swali La 21:
## Jee, Ndugu Branham alifundisha Kuowa wengi?

**Jibu:** Hii niswalii gani katika duniya ya watu! La! Haija kuweko, sivyo. Wandugu wengi katika inchi za Afrika, ambapo kuowa wengi ikingali nafanyika wakiweka mkazo ku maneno ya nabii kuhusu hiyo, ili wapate namna ya kuweza kutimiza tamaazao. wakijilinganisha na Ibrahimu, Yakobo, Elkana, Gideoni, Daudi na Salomono nawengineo wakiweka mkazo na kusema kwamba Daudi alifanya dhambi moja yauzinifu alipo muchukuwa mke wa Uriya. Somo hili nilakushika naangalisho kuliko zengine kwakuwa linaele weka haraka vibaya.

Ndugu Branham alisema kuhusu hiyo"lakini sasa mihuri ilipo vunjwa Roho wa kweli anatuongoza kwenye neno. Hiyo ina tuonesha kwa nini makosa yote yalionekana katika vizazi vyote ni kwa sababu mihuri ilikuwa bado haiya vunjwa. Ilikuwa bado kufunuliwa. Hii ni kweli" (Ndoa na Talaka Pg. 34)

Ndugu Branham alitumikisha mara moja moja msemo "polygamie" yaani "kuowa wengi" Zaidi sana katika mahubiri yake yanayo itwa "Ndoa na Talaka" ya (siku 21 Februari 1965 akilinganisha na Agano la kale. Hakuwa na itaji ya kuweka mzigo kwa wa ndugu. Wakati Mungu alitowasheria hakutia sababu. "*Akimuchukuwa mwengine…*" si wake wengi (Kutoka 21:10). Kwa njia hiyo, Mume angeshika usimamizi wote kwa kila mmoja wao. Bwana Mungu naye aliweka haki ya mzaliwa wa kwanza kwa hiyo (Kumbukumbu 21:15-17).

Mtume Paulo aliandika waziwazi kwamba kila mume anastahili kuwa na muke wake na kila mwanamke anastahili kuwa na mume wake (1. Wakorintho 7). Ndugu Branham kwa musemo muzuri alitafuta kuweka mkazo ya kwamba mwanamke aliumbwa kwa ajili ya mwana mume, siyo mume kwa ajili ya mwanamke (1. Wakorinto 11:9) Na ndiyo sababu, baada ya Talaka Mume anaruhusiwa kuowa tena, bila kuonekana kama mwenye makosa mbele ya mkewe alie mtaliki. Lakini sasa kama mwanamke huyu akiolewa tena, anaishi katika uzinifu, kwa sababu anafungwa na sharia ya Mungu kwa kiapo chake cha ndoa wakati wowote mume wake angali hai (Waroma 7:2, 1. Wakorintho 7:39). Hiyo ilifunuliwa kwa ndugu Branham kwahiyo wingu ya kimaajabu ya Rangi ya kimanjano iliyo mufikia wakati wa kufunguliwa kwa mihuri saba. Tazama maneno ya kinywa chake; "Hapa haisemi kitu chochote Zaidi yake anaye owa tena, bali kwa mwanamke … Hapa inasemeka kwamba anaweza kuowa tu bikira, lakini hawezi kuowa mke wa mwengine.

Sivyo na sivyo. Na akiowa mke alie talikiwa, anaishi katika uzinifu … Kwasasa tambueni ya kwamba mume anaweza tena; lakini mwanamke hawezi. Kama David, kama Salomon, kama vile mwendeleo ya biblia yote…“ Tofauti inaonekana wazi! “Mwanamke anapashwa kubaki pekee yake bila kuolewa tena ao anaweza kujiunga tena na mumewe. (1. Wakorintho 7) Hastahili kuolewa tena anapashwa kubaki peke yake. Lakini sasa tazameni hakusema hivyo kuhusu Mume. Mnaona hamuwezi mkadanganya neno“ (Ndoa na Talaka Pg. 33-33).

Wote wangeweza kuelewa somo hili kupitia maelezo yaliyo wazi ambayo ndugu Branham ametoa kwa kuwa alipokea jibu ya hapohapo ya Mungu kuhusu shida ya Ndoa na Talaka. Hii ufunuo inayo tembea na maandiko ikotofauti sana na yale ambayo tuliyo ya pokea katika mawazo ya kitamaduni nayale ambayo madhehebu yanafundisha. Yule ambaye anaye jiwazia kama anajua yote kuhusu soma hili anapashwa kujiachilia aambiliwe kwamba Mungu hawezi akamwongelea mtu kama huyo. Jambo hili lilikuwa la muhimu sana kwa Mungu mwenyewe katika wingu la kimaajabu kumupa mtumishi wake na Nabii ufunuo kamili. Wote wanao jitangazia kweli kuwa wanaamini ujumbe wa wakati, wataheshimu hilo.

## Swali La 22:
## Unafundisha je kuhusu Ndoa na Talaka?

**Jibu:** Sina fundisho langu mwenyewe kuhusu somo lolote. Musa, BWANA wetu, mtume Paulo na ndugu Branham walifundisha kuhusu somo hili kwa urefu. Kwa hivi hakuna mtu anaye itaji kuandika tena kuhusu somo hilo isipokuwa kuweka kwa utaratibu yale ambayo yaliandikwa kuhusu somo hilo.

Ni kama vile ndugu Branham alikuwa akisema; Nishida ya kale ambayo ni ngumu,“ambayo hauwezi kuijuwa mpaka ifunuliwe kwako. *“wakati bwana Mungu Alipana maagizo hakuisahau somo hili la muhimu kwa kuwa alikuwa akisema kuhusu Uzinifu … usimtamani mke wa mwenziyo…“* (Kutoka 20).

Katika mahubiri kwenye mlima (Mathayo 5:27-32) Bwana wetu aliongea vile vile kuhusu hiyo; *„Usizini…yeyote anaye mtazama mwanamke na kumutamani amefanya uzinzi pamoja naye moyoni mwakwe“*. Na kwa hiyo aka ongeza: *„jicho lako la kuume liki kukosesha, liongoe ulitupe mbali nawe… Na mkono wako wa kuume*

*ukikukosesha ukate uutupe mbali nawe…"* Pia alisema kuhusu mume anaye weza kuachana na mkewe isipo kuwa sababu ya uzinifu. Kwa namna hiyo amemuleteya muke wake kuwa muzinifu ikiwa ana olewa, na kwa hali kama hiyo mume ndiye ata kuwa musimamizi.

Katika ma kabila yote na ukoo hapa duniani, ndoa ina heshimiwa kamasehemu ya maisha ya familiya. swali linalo waka moto ni; Uzinifu ni nini kulingana na sheria ya Mungu mahali wawili wakaweza wakafa? Maandiko ina sema nini? Uzinifu ni wakati mume anakuwa katika kitendo cha ndoa na muke wa mume mwengine *„Mume akipatikana akilala na bibi aliye na mume, hapo wata kufa wote wawili"* (Kumbukumbu 22:22).

Katika Malaki 2, Bwana wetu ali laumu kwanza makuhani na kabila la walawi sababu ya mafundisho yao ya uongo. Hapo tena aliongea kuhusu agano za Baba zetu, ambao Yuda alifanya kitendo kiovu kwa kuoa ma binti za miungu ya mataifa. Sehemu hii ya unabi ni ya kilindi sana na ina tuongoza kwa lengo la muhimu,"kusema aweze kutafuta mbegu ya Mungu…" mbegu hiyo ime ahidiwa kutoka shamba la Edeni ambao ni Kristo (Wagalatiya 3:16). Baada ya hiyo tuna soma kuhusu talaka ambacho ni kitendo cha ukatili. wakati mume ana mtaliki mke wa ujana wake hapo ana vunja agano pamoja naye (shahiri la ine). Haija wayi kuwa katika mafikiri ya Mungu kwa muke kutaliki mume wake kama vile Israeli hainge weza kutaliki Mungu, hapo ina andikwa kwa shida kama hiyo mume ana weza kumupa mkewe baruwa ya talaka, lakiini mwanamke hawezi kutoa baruwa ya talaka kwa mume wake.

Nukuu: „kama mwanamke anaweza kutoa baruwa ya talaka kwa mume wake hiyo ni shetani" (C. O. D, Vol 2 Page 81)(English) maswali na majibu.

Mbele mume ao mke kuwaziya talaka, hii ita endeleya kuwa ushuhuda wangu: ni vema huyu mume ao mke awaziye kama ana weza kujikata mkono ao mguu ili apate kufikiriya kwenda kwa mahakama kuomba baruwa ya talaka. Talaka ni kitendo cha mauwaji kwa msemo kamili, wakati nguvu zote za kishetani za chuki zina onekana. Haivunji ndoa pekee, bali ina vunja piya jamaa, kanisa na jamii. Hakuna kitendo cha ukatili cha shetani kama talaka ni mauwaji ya maisha. Kwa kuifunika na majani ya mitini kama kanzu ya uhaki ya kibinafsi ni kama mazihaki.

Shetani mudanganyifu hujificha nyuma ya kila kitu cha ubishi kinacho tokeya. Mwanamke anapo kataa na kumuacha mume wake ana jikata kichwa chake yeye mwenyewe kwa wakati huo ana poteza uongozi wake wa kiroho na wa kimwili na hapo ana jazwa sumu ya ulimi kwa sababu ametoka chini ya utaratibu wa kiungu kuhusu ndoa, jamii na maisha ya kanisa. Kwa wakati huo ana fanya dhambi za makusudi na kumusulubisha mwana wa Mungu upya, na kuhayarisha mwana wa Mungu hazarani akifikiri kwamba anajiliipiya ubaya na kubomowa mume wake.

Matendo yanayo onesha yule alie na makosa ni haya: Hakuna Rehema, hakuna musamaha, hakuna uambatanisho ila mastaka tu, uadui isiyo chunguzwa inayo zidi kupita mauti.

Kwa wakati moja huyo mtu huleta sababu zake binafsi za kukubalisha ili atulize hukumu ya zamiri yake na kuleta mastaka yake ya uongo mbele ya familia na waamini na watu wote kwa ujumla.

## Swali La 23:
## Jee, ni vipi kuhusu yale yanayo husu familia ya mutumishi wa Mungu?

**Jibu:** Tunaweza kuuliza swali, maandiko inasema nini kuhusu jambo hilo? Kwa mfano katika Mathayo sura 5, 6 na 7 katika mahubiri kwenye mlima Bwana ameweka yote. Kwa mwisho wa mahubiri hayo tuna soma maneno haya*: „Ikawa Yesu alipoyamaliza maneno hayo makutano walishangaa mno kwa mafundisho yake,“* (Mathayo 7:28) Katika matayo 10, Bwana anawaambiya wanafunzi kumi na wawili aliyo waita mitume na siyo makutano. Akawaambia; *„Na mtu asipo wakaribisha wala kuyasikiliza maneno yenu, mutokapo katika nyumba ile au mji ule, kunguteni mavumbi ya miguu mwenu.“* (Mathayo 10:14). „Angalieni, mimi na watuma kama kondoo kati ya umbwamwitu, basi iweni na busara kama nyoka na kuwa watu wapole kama hua.“ (Mathayo 10:16). *„lakini watakapo wafukuza katika muji huu, kimbilieni mwingine, kwa maana ni kweli na waambia; Hamtaimaliza miji ya Israel hata ajapo mwana wa Adamu“* (Mathayo 10:23) kwa mwisho aliandika kuhusu utume wa watumishi wake kwa maneno ya fuatayo; yanayo dumu milele: „*Awa pokeaye nyinyi anipokea mimi, naye aliye nituma*“ (Mathayo 10:40). Wote wangeweza kusoma kwa makini yale

Bwana anasema kwa wale aliyo watuma yeye mwenyewe. Wana pashwa kwenda mji kwa mji wakiwa wameowa au wasiwe wameowa.

Mwito ni agizo kwa wale ambao BWANA wetu Yesu Kristo aliyo waita ili watangaze usalama, anasema: *„msidhani yakuwa nimekuja kuleta Amani duniani: la! Sikuja kuleta Amani baali upanga. Kwa maana nilikuja kumfitini mtu na babaye, na binti na mamaye, na mkwe na mkwe mtu; Adui za mtu ni wale wa nyumbani mwake.*“ (Mathayo 10:34-36). Hiyo ni machafuko katika familia iliyo tangazwa mbele ambayo inaweza fanyika hata ndani ya nyumba ya muhubiri. Hata hivyo, mtumishi wa Mungu anapashwa kuendelea kuhubiri kwa wale ambao aliwatuma, hakuna maisha ya familia bora ao huduma yenye haina vita. Mungu hakusema kwamba mtume nabii au mwalimu awe mume alie oa. Hali yoyote ndoa ya mutumishi wa Mungu anaye weza kuwa nayo, Anapashwa kuheshimu utume wa kiungu.

Tazama ginsi ilivyo tofauti na maneno ambayo yana sema kuhusu wazee wa kanisa la pahali! Kufwatana na 1. Timotheo 3 na Tito 1, wazee na mashemasi wanapashwa kuwa wameoa, musemo“Awe Bwana wa mke mmoja…“ (1. Timotheo 3:12). Haimaanishi ya kwamba wengine wawe na wanawake wengi, ginsi wanavyo taka. Hiyo ina maanisha ya kwamba mume yeyote anaye kuwa na usimamizi Fulani ndani ya kanisa la pahali anapashwa kuwa ameowa kwasababu anapashwa kutatuwa mashida ambazo zinazo zuka katika familia za kanisa la pahali.

**Nukuu: „**Biblia inaagiza shemasi awe mume alie na mke. Anastahili kuwa mume wa mke mmoja“ (C. O. D P. 354).

Ninamna gani kwa mwana wa Mungu? Ingawa huduma yake yakimbigu ilishuhudiwa kwa kuzidisha mkate na kuponya wagonjwa wengi na kufufua wafu na kutuliza zoruba, etc…lakini ndugu zake hawakumuamini (Yohana7; 5) wali mtambua kwa kimwili, lakini kwa kiroho hawa kumutambua. Tuna soma katika Mathayo 13:53-58 kwamba mwana wa mtu hakuweza kufanya kitu chochote katika mji yao sababu ya kutoamini kwao. Walisema: „Huyu si mwana wa seremara? Mama yake si yeye aitwae Mariamu? Tunajua na ndugu zake…, na baba zake si wanaishi hapa kwetu? „na wali kwazika sababu walimuhukumu kutokana na yale ambayo wali ona kwa macho yao nayale ambayo watu walisema. Hapo juu Bwana anasema*: „Nabii hakosi kupata heshima isipokuwa katika nchi yake na nyumbani mwake*

*mwenyewe"* (Mathayo 13:57b) Hii ina tuletea uzuni tunaposoma maneno ambayo wale viongozi wa kidhehebu waliyo yasambaza kuhusu Bwana wetu na mkombozi wetu kwa wakati wake. Mafarisayo na waandishi walimuambia mbele yake " *sisi hatukuzaliwa kwa zinaa …, je sisi hatusemi vema ya kwamba wewe u musamaria na wewe una pepo?"* (Yohana 8:41, 48). Fikiriya kwa hiyo kwa muda: Bwana wetu aliezaliwa na Mungu, aliitwa musamaria na kuzaliwa katika zinaa! Hapo ndipo alipo sema: *„…kwamaana nilitoka kwa Mungu nami nime kuja…nyinyi ni wa baba yenu shetani…"* (Yohana 8:43-44).

Mtumwa anaweza kutendewa mambo tofauti na Bwana wake? Inaonesha kwamba mkombozi hakuja kuunda familia ya kidunia, ama kufanya huduma yake kuwa biashara ya kupata ndani faida. Hilo ndilo jambo linalo fanyika kwa watumishi wake. Watumishi wa Mungu wana mwito uliyo juu sana kwa ajili ya mwili wa kristo ni mwito ambao ni tofauti na familia za kimwili.

Hakuna ahadi katika neno la Mungu kuhusu wa mtoto wa nabii ao mtume, ao mwalimu ambao anaweza kurithi kazi ya kiungu. Nabii Samuel aliwaza vizuri wakati alipo weka watoto wake wawili kuwa waamzii, lakini: *„wanawe hawakuenda katika njia zake baali waliziacha ili wapate faida. Wakapokea rushwa na kupotosha hukumu"* (1. Samweli 8:1-5). Hata maamzi ya nabii ana yoweza kuamua akiwa na itaji nzuri inaweza kushindwa ila tu maamzi ya Mungu haiwezi kushindwa. Inaweza fika hata wakati mtoto wa nabii ao wa mufalme, ao wa mutu wa Mungu anaweza kujiinua na kujipatia cheo Fulani na kuvutia watu nyuma yake. Tunayo mfano kama huu katika 1. Wafalme 1, wakati Adonia mwana wa Daudi kwa Hagai*,"Alijiinua na kusema: mimi nitakuwa mufalme…na Akatayarisha magari za vita na mafarasi na wanaume makumi tano mbele yake"* maamzi ya Mungu ilikuwa amekwisha amuru kwamba Solomono ndie atafwata kukuwa kwa kiti cha Daudi. Lakini kwa macho ya ndugu yake hawa kuwazia kama anaweza kuwa mwenye kiti. Inawezekana watoto wanaweza kujiambia wengine eti: „Nitakuwaka Raisi" „Nitakuwaka muongozi!";"Nitashika usimamizi!""mimi nitakuwaka na kusanya mikutano na nitakuwa na kusanyiko"."Ni nataka…","Ni nataka…" Tangu mwanzo wa nyakati, kila mtumishi wa kweli wa Mungu alitimiza wito wake aliopokea bila kuona hali na Mungu hakujuta wito wake. Hakuna mtumishi wa Mungu aliye wai kusema: „;Ni nataka…""Ninataka nifanye hiki ao kile!"wengi kati yao hawa kupenda waende lakini wali kazwa kwenda

kwa sababu mwito wa Mungu hauna majuto. Ambao hata awe na familia wala asiwe nayo: kutumwa kwa kiungu ni sehemu ya mpango wa okovu wa Mungu yenye inapashwa timizwa. Haidhuru kwa hali gani.

## Swali La 24:
## Ninamna gani kuhusu kitabu cha nyakati saba za kanisa?

**Jibu: K**wa April 1966, nili kuja na vitabu viwili vyakutoka marekani"Nabii wa karne ya makumi mbili, kizazi cha kanisa la Laodikia, pia na kitabu chamaelezo kuhusu vizazi saba vya kanisa". Niliwazia kwamba ndugu Branham yeye ndie alie andika kitabu cha vizazi vya kanisa na mimi nili kitafsiri katika lugha ya kijerumani na kukizidisha ndani vitabu 10000. Natena nili gundua jinsi kartasi 48 za kitabu"kizazi cha kanisa la Laodikia"kuanza neno la kwanza hadi mwisho kunapatikana ndani kwa kartasi 319 hadi 365 katika kitabu cha kingereza kuhusu vizazi vya kanisa. Mwisho nili elewa jinsi katika ujumbe ambao ndugu Branham alihubiri na yaliyo andikwa katika kitabu"maelezo kuhusu vizazi saba vya kanisa"kulikuwa tofauti kubwa na hata katika kitabu hicho kulikuwa mafundisho yasiyo ya kibiblia ambao ndugu Branham haku hubiri hata kidogo. Kwa mfano katika kitabu hicho kunaandikwa kwamba, watu wenye bado hawajazaliwa upya wataingia katika uzima wa milele sababu ya mambo mema waliyo watendea wandugu. Hii inapingana sana na 1. Yohana 5:11-12: *„na huu ndiyo ushuhuda yetu ya kwamba Mungu alitupa uzima wa milele; na uzima huu umo katika mwanawe. Yeye aliye naye mwana anao huo uzima; asiye naye mwana wa Mungu hana huo uzima!"*Mufano mwengine ni ya matafsiri yasiyo ya kweli kuhusu mti ya uzima na mti ya kujulisha mema na mabaya. „…kwamba wenye haki na waovu wako karibu karibu katika bustani…Na bila mashaka matawi yake nayo ina karibiyana". Siyo mara moja kitabu hiki hakitofautishe mataifa iliyo katika matayo 25:31, yenye itapatikana mbele ya utawala wa myaka elfu na hukumu ya mwisho mbele ya kiti cheupe itakayo fanyika baada ya myaka elfu katika Ufunuo 20:11. Nina kataa kutumia nukuu tofauti zilizo katikz kitabu hicho zisizo za kweli. Ninaomba kila mmoja kutumia ujumbe halisi. Nilipo omba kitabu hicho niliambiwa kwamba ndugu Lee Vayle ndie alikuwa mwandishi wakitabu hicho cha vizazi vya kanisa. Ndugu Branham alisema ya kwamba hajasoma kitabu hicho hata siku moja. Katika mahubiri yake yanayo

sema „Mutu anaye kimbia toka machoni pa Bwana“ambao alihubiri tarehe 17, Februari 1965. Alisema „na sasa kuna kitabu cha Nyakati za kanisa nina waza kwamba ndugu wetu mpendwa amepata uvivio kidogo ya namna Fulani, kwa sababu alisema kwamba ameandika vitabu viwili yeye mwenyewe. Na hapo aliandika kitabu kinacho itwa ninaamini,“Nabii wa karne cha ishirini „na“Nyakati ya kanisa la Laodikia“sija soma vitabu hivyo mwenyewe. Ikiwa nina weza kusoma vitabu hivyo yawezekana nina weza kubadilisha maoni yangu kuhusu hiyo…“ Sababu ya mafundisho ya kitabu hicho yasiyo eleweka isiyo ya kimaandiko matakatifu. Kinaweza kutumikishwa kama kitabu cha historia lakini hakiruhusiwe kuhusu kazi ya mafundisho.

## Swali La 25:
## Jee, Muda za Nyakati za kanisa zilimfunuliwa ndugu Branham?

**Jibu:** Hakukuwa lazima kuweko ufunuo kuhusu nyakati za vizazi vya kanisa. Ndugu Branham maranyingi alisema kuhusu mtu wa historia Dr Clarence Larkin. Katika kitabu chake“Dispentional Truth“tunakuta kwa kartasi yake ya 130 na 131 masehemu za kuenea, ginsi ndugu Branham alivyo ziandika. Ila kuhusu majiona za wajumbe ndugu Branham mwenyewe ndie alie zichagua. Nilitosha huko Jefelsanville chapo hilo la vizazi vya kanisa na majuma sabini za Danieli ambalo ndugu Branham alikuwa amechapa kwa ajili ya mafundisho kuhusu somo hizo. Hiyo inaonyesha wazi wazi kwamba fundisho lake lilikuwa kuhusu somo hili, kulingana na ushuhuda wa maneno yake.

## Swali La 26:
## Jee, Ndugu Branham alitabiri kwamba mwisho wa dunia ni katika mwaka wa 1977?

**Jibu:** APANA**,** Ndugu Branham haja wai fanya unabii kama huo. Ijapokuwa katika mahubiri yake mengi alikuwa akisema kuhusu mwaka 1977, maneno haya yanayo patikana katika kitabu cha vizazi vya kanisa (page 322) haikutokea kinywani mwa ndugu Branham, hata hayakupatikana katika mahubiri zake zilizo shikwa kwenye kanda. Ila maneno hayo yalitokea kwa maandishi ya ndugu Lee Vayle mwandishi wa kitabu hicho. Maneno hayo tena yanaweza patikana kwa ukurasa wa 7 wa kitabu kinacho itwa“kanisa la kizazi cha

Laodikiya“chenye kuwa na ukurasa 48, Tarehe 17 januari 1972 Lee Vayle alijibia swali langu kuhusu mwaka 1977: „nina amini pamoja na nabii ya kwamba katika mwaka 1977 mambo yote yatafikia mwisho wake na tuchukuliwe katika myaka elfu“Hii inaonekana wazi kwamba ilikuwa maoni ya huyo mwandishi, lakini si ya nabii.

## Swali La 27: Jee, ndugu Branham aliona kalendari inayo isha kwa mwaka 1977?

**Jibu:** APANA, kwa kujua kwangu hakuna mtu hata mmoja alie ona maneno inayo lingana na kupata ono kutoka kwa ndugu Branham. Na leo hakuna mtu anaye weza kuamka na kushuhudia historia hii duniani. Nikatika mwaka wa 1966, tulipo sikia mara ya kwanza maneno kuhusu“ONO la kalendari“la ndugu Branham. Baada ya hayo ndipo ono la kalendari lili sambazwa na mimi pia niliandika katika barua yangu ya mzunguko ya Februari 1967 kuhusu hiyo. Tena hapo ndipo nilianza kuwa na mashaka kuhusu mwaka 1977 na kama vile nilionyesha mara nyingi niliuliza ndugu Lee Vayle ufafanuzi kuhusu“ONO la kalendari“kati hiyo barua moja ya januari 1972 alijibu yafwatayo kuhusu ONO la kalendari,“Sasa ndugu Frank, kulingana na watu waliyo tangaza kwamba ndugu Branham aliona kalendari ikiwa mikononi mwake na ikifunguliwa mpaka mwaka wa 1977. Bila mashaka hapa tuna kuta kwamba haikukuwa ono la ndugu Branham, baali ilikuwa kitu Fulani ambacho mtu Fulani ali jiundia, tuliongelea kuhusu jambo hili…“ Tunaendelea kuona ya kwamba wasimamizi wa Marekani hawaja wai kukosowa hiyo utangazaji wa uongo kuhusu mwaka 1977 na mpaka uongo huo unaendelea wa kiutilia ndugu Branham. Hapo maadui zake wamepata namna yaku tumia maneno hayo waki muiita nabii wa uongo wakisema kwamba unabii haukutimia aliyo utabiri kwa ajili ya faida zao wenyewe.

## Swali La 28: Jee, Ubatizo wa roho mtakatifu ni sawa sawa na kuzaliwa upya?

**Jibu:** La: maneno hayo yaliyo katika kitabu cha nyakati za kanisa, haikutoka kinywani mwa ndugu Branham baali kwa mwandishi wa

kitabu na ndio sababu hata haipatikani hata katika mahubiri yaliyo shikwa kwenye kanda na tena haiko maandiko. Moja ni kuzaliwa upya na roho mtakatifu na ingine ni kujazwa na roho mtakatifu. Katika matendo ya mitume 8, watu wali amini kupitia mahubiri ya mwinjilisti Filipo na kubatizwa. Hapo mitume walikuja toka Yerusalemu kuwaombea ili wapate kupokea roho mtakatifu. Katika matendo 10, walio amini wali ishi ujao wa okovu, walitubu, wakasemehewa dhambi, wakahesabiwa haki, kuzaliwa upya na ubatizo wa roho mtakatifu. Kupitia kuzaliwa upya tuna kuwa wana na binti za Mungu kupitia ubatizo waroho mtakatifu tuna wekwa kama viungo vya mwili wa kristo na kupokea nguvu ya kazi (luka 24, 47matendo 1:8, matendo 1, 1. Wakorintho 12:1, 14 etc) yamuhimu ni kuishi hatuwa hizo mbili, hata kama zinaweza kuja kwa mara moja ama tofauti lakini lisiwe ndiyo jambo la kuleta mabishano lakini liwe mazoezi ya kuishi kwa kila mtu binafsi kupitia rehama ya Mungu. Ndugu Branham alisema: „Unapo amini Bwana unapokea mawazo mapya maisha mapya lakini bado haija kuwa ubatizo wa roho mtakatifu. Unaona? Mwaweza kupata kuzaliwa upya wakati munapo amini ; mume pokea uzima wa milele…lakini ubatizo wa roho mtakatifu una kuingiza ku mwili wa Kristo na kupewa zawadi kwa kufanya kazi“ (COD p269, 363, 364).

## Swali La 29:
## Jee, Ni namna gani kuhusu ono la ndugu Branham katika hema?

**Jibu:** Nilisikia mara ya kwanza kwa mwaka wa 1958 kuhusu“ONO katika hema“ambayo ndugu Branham aliona kwa mwaka 1955. Ni Roy Borders aliekuwa akitayarisha mikutano ya ndugu Branham, alie kuwa na itaji yangu alinijibu tarehe 18, mayi 1965 karibu;“…Nitajaribu kujibu kwa maneno machache kulingana na jinsi niliambiwa na ndugu Branham…kuhusu hema inawezekana kwamba Hema litatumiwa katika Ulaya na katika inchi nyingine inje ya Marekani…“ Ndugu Branham alikuwa akitarajia utimilifu wa“ono katika hema“mpaka mwisho. Lakini tangu alichukuliwa nyumbani, jambo hilo halikusikilikana tena. Kwa nyakati hizi mambo mengi yame kwisha hubiriwa na wahubiri tofauti ili waweze kupigania mafundisho yao wenyewe. Kuhusu ONO katika hema wamoja wanafundisha kwamba ndugu Branham atafufuka na kuendelesha huduma yake

katika hema kwa muda kidogo. Shida ni kwamba mambo hayo yana endeleshwa na wandugu wanayo jificha nyuma ya ndugu Branham na mafundisho yao wakiwa chini ya ushawishi mbaya kwa namna nyingine hawange weza kuvutiya watu nyuma yao. Hii ninaisema kama neno la Bwana katika jina la Yesu Kristo wakati hakuna ahadi ya kitu Fulani katika neno la Mungu hapo hakuna utimilifu pia. Hiyo ndiyo ukweli.

### Swali La 30:
### Jee, kitu chochote kilicho oneshwa katika ono chaweza kubaki pasipo utimilifu?

**Jibu:** Inaeleweka vizuri jinsi kwa wakati wa ndugu Branham alipo kuwa angali hai, watu walingojea utimilifu wayale yote aliyo yaoneshwa katika maono. Lakini yawezekana ono linaweza kuwa limetimilika wala kutimilika kwa namna nyingine tofauti na namna walivyo kuwa wakingojea. Ndugu Branham alisema mara mia kuhusu"Hema" akiilinganisha pamoja na Abraham na sara mpaka kufunguliwa kwa mihuri kwa mwezi ya machi 1963. Alikuwa akifanya hivyo alipokuwa akianza maombi kwenye mustari akionyesha kwamba alama hiyo yenyewe ilijirudia kwa wakati wetu katika Mwanzo 18, Hema ina semwa mara tano, Sara alikuwa katika Hema, wakati Bwana Mungu alipotoa Ahadi ya kuzaliwa kwa Isaka, wakati wa mustari wa maombi ndugu Branham alikuwa akigeuziya watu mugongo wake ili aweze kutambua kwamba Mungu Yule Yule yuko hapo, yeye anaye jua na kufunua siri za mioyo kama vile ilivyo fanyika kwa wakati wa Abraham, sasa ninaonya kila mmoja ili asiyifanye kuwa fundisho Fulani kwa kuwa ni vizuri tuache mambo yote kwa Mungu.

Inawezekana mambo ya kiroho ionyeshwe kwa mfano ya kimwili kama vile kwa mfano ndugu Branham alivyo jiona katika ono akichukuwa katika kanisa kila aina ya mboga, lakini maana ya kweli (tafsiri) lakweli lili kuwa ni chakula cha kiroho, neno lililo funuliwa kwa wakati wetu ambayo lingeli wekwa katika gala. Mutume Petro naye pia aliona katika ono kwenye kitambaa kila aina ya nyama na mandege etc. Tafsiri ya kiroho ilikuwa ni kwamba okovu ya Mungu ilikuwa inageukia mataifa pia (Matendo 10:9-22) Bwana wetu naye alionyesha mambo ya ufalme wa Mungu katika mifano na maneno ya vitu vinavyo onekana. Hapo ndipo alitangaza"mambo yaliyofichwa tangu musingi

wa ulimwengu" (Mathayo 13:34-35) Wandugu waliyo endelea kungojea utimilifu wa ono katika hema pamoja na ndugu Branham hakuna ahadi hata moja katika Biblia kuhusu hiyo. Hata katika maandiko matakatifu hatuna mfano wanabii mmoja alie fufuka na kuendelesha huduma yake. Nakwasababu hiyo, si ya kushangaza kuona wandugu kama hao hawawezi kuwa na itaji ya kuwa na ushiriki pamoja nasi kwa sababu sisi tuna pashwa tangaza wazi kwamba huduma ya ndugu Branham ili isha wakati ali chukuliwa katika utukufu. Kwa kuwa hawa kubali kitendo hicho wana kataa pia Yule ambae anatangaza kuwa amepewa mzigo na Mungu wa kuchukuwa ujumbe kwa mataifa wakimustaki kuwa mudanganyifu wa kupoteza bibi arusi na kuwa yeye ni Antikristo, kwa kuwa wanamuwazia kuwa"Anapinga Nabii"na kupinga mafundisho yote ya ngurumo na matokeo ni kukataliwa kwakuwa wao wana sema: „kwamba hakuna mtu anayestahili kusema ya kwamba ametumwa kupeleka ujumbe waneno lililo funuliwa kwa mataifa"sababu maoni yao ya kimafundisho inasema kwamba mambo yote yalikwisha pamoja na huduma ya ndugu Branham yote yalimalizika naye."na hapo kwa muda"wana tumia mabishano yasiyo na mafaa wakitumia yale ambao nabii alisema na kusambaza mafundisho yao kwa namna isiyo faa.

Wanatumiya manukuu za ndugu Branham wakizigeuza kwa namna isiyo ya kweli. Ni njia gani ya maendeleokatika ujumbe! Kwa kweli matumaini kama hayo haina uhusiano pamoja na injili ya Yesu-Kristo. Bwana wetu Yesu hatajwi hata mara moja katika yale wanayo yatangaza na kungojea kwamba yatatimia, Matumaini ya uongo ambayo wamejishibisha wenyewe kwa mwisho itawapatisha haya na kukata tumaini, nina wasihi ndugu wapendwa ya kwamba mambo yote yanayo husu ufalme wa Mungu hayana uhusiyano na tafsiri ya mtu binafsi. Hapa tunataka tuangalie Musa na utume aliyo upewa kuongoza watu mpaka inchi ya ahadi, Hakuruhusiwa kuingia pamoja na kanisa la Islaeli. Kulingana na kumbukumbu la torati 34; aliruhusiwa kuona inchi yote akiwa juu ya mlima Nebo, lakini asiingiye ndani. Pamoja na ndugu Mehnert nilichukuwa taxi kutoka Amman na tulienda kwenye mlima Nebo tuliona mambo ya kushangaza kwa upande wetu wakulia tuliona Yeriko na kwaupande wa kushoto tuliona Enguedi na bahari ya kufa na mbele yetu Yerusalemu. Ninaweza kuya elewa namna gani yale ambayo Musa alishindwa! Kwa hivi njia za Mungu ni juu sana kwa ufahamu wetu. Kwa maoni ya mwili inaonekana kama Musa alikuwa hakumaliza kazi ya utume wake! Tunaitaji kuelewa kwa

kiroho ili tuweze ku heshimu njia za Mungu na mipango yake. Tunaamini kwamba Mungu mwenyewe atamaliza kazi yake ya ukombozi kama vile alivyo panga kabla yakuwa musingi ya ulimwengu. Jambo la muhimu ni kubaki katika neno la Ahadi na kupata sehemu kwahiyo kwa sababu Imani ya kweli inapatikana tu katika maahadi za Mungu. Kulingana na maahadi za Mungu inaandikwa „*Halikukosa kupatikana neno lolote katika ahadi zake njema aliyo ahidi kwa mkono wa Musa mtumishi wake*“ (1. Wafalme 8:56). „*Maana ahadi zote za Mungu zilizopo katika yeye ni ndiyo tena kwa hiyo katika yeye ni Amina. Mungu apate kutukuzwa kwa sisi*“ (1. Wakorintho 1:20). Wakati wakuja kwa kwanza kwa Kristo nabii aliye ahidiwa ndie alie kuwa mtangulizi lakini Bwana mwenyewe alitimiza kazi ya ukombozi hapo msalabani kalvari, hivyo ndivyo ilivyo hata sasa ndugu Branham alikuwa nabii alie ahidiwa kupitia yeye mambo yote yangepashwa kurudishwa tena kwa upya na kuyarudisha kwa na fasi yake halisi. Ujumbe ndiyo mtangulizi lakini ni Bwana mwenyewe ambae ata imaliza kazi ya ukombozi „*maana Bwana atatimiza kazi yake Duniani bila kukawia kwaufupi katika utakatifu wake*“ (Warumi 9:8).

## Swali La 31:
## Tunaweza kulinganisha namna gani Islaeli na kanisa?

**Jibu:** Jibu la swali hili lina kutaniwa katika Matendo sura 15:13-18. Kwanza Mungu ana tembelea wa mataifa kwa neema yake ili kuwaita kutoka kwaajili ya jina lake. Baada ya hii atageukia Islaeli ili kuijenga upya nyumba ya Daudi. Nanihivi alivyo sema mtume katika waroma 11 akishuhudia maneno hayo katika sura hiyo yote. Tuna maoni kwa ujao kuhusu mpango wa okovu, pamoja na wayuda na mataifa kuhusu Islaeli na kanisa. Alama ya muhimu ni kwamba kabila 12 walitoka katika inchi 143 wakirudi kwa inchi ya ahadi. Kwa sababu gani? Kwa sababu wanastahili kubaki katika Yerusalemu ndani ya Islaeli, Ili wawekwe muhuri wakati wa huduma ya wanabii wawili (Ufunuo 7:1-8, Ufunuo 11): kwa namna moja waamini wote wa kweli walio sambazwa katika madhehebu za kiKristo watakusanywa na kuongozwa kwenye neno la ahadi la sasa na kuwekwa muhuri wa Roho mtakatifu (Waefeso 1:13). Kama si hivyo hawataweza kushiriki kwa unyakuo. Imani isiyo na Ahadi ya Mungu kama msingi ni mawazo za kidini. Imani ya kweli inafungwa katika maahadi za Mungu. Kama vile Ibrahimu alivyo ami-

ni yale ambayo Bwana alimuahidi na baadae aliona utimilifu wake. Hivi ndivyo mbegu halisi za Ibrahimu zinavyo amini maahadi za wakati huu na wataona utimilifu wake.

### Swali La 32:
### Kulingana na mpango wa okovu tuko katika sehemu gani?

**Jibu:** Tuna fika sasa kwa sehemu ya kizazi cha kanisa katika kizazi cha Bibi Arusi, kurudi kwa Yesu-Kristo ni karibu sana. Tunaweza kusema hivi tukiona maalama za nyakati na unabii wa kibiblia vilivyotabiriwa mbele ambavyo vina endelea kutimia zaidi sana pamoja na Islaeli. Ujumbe wa wakati wa mwisho niya muhimu sana ambao ni sauti ya usiku wa manane. Nimwito wa kuita kutoka kwa wote ambao wana sehemu ya kanisa Bibi-arusi. Yale ambayo mtume Paulo alishuhudia kwa wakati yake yanafanyika tena kwa sasa.*"Basi ni vivi hivi wakati huu wa sasa kuna mabaki walio chaguliwa kwa neema*" (Warumi 11:5). Ni wale tu watakao rithi vyote kwasababu wanasikia na kufuata na kuweka katika matendo yale ambayo Roho ayaambiayo kanisa. Na Mungu atamaliza kazi yake hapa Duniani, kwa ujao wa nguvu yake ya ajabu ambayo inaitwa kurudishiwa kwa ujao kwa mambo yote. Sehemu ya hii ni hudma ya neno lililo nenwa na kitendo cha ajabu cha Roho ambacho kitaongoza mpaka kuonekana kwa mwana wa Mungu na ufufuko wa wafu. Na lengo la muhimu katika haya ni kurudi kwa Yesu-Kristo.

## KWA MAFUPI

Kwa furaha kubwa nina tazamanyuma kwa miaka 54 ya kuhubiri Injili na miaka 43 katika hudma Duniani pote, miaka ambayo nilipata neema ya kuchangia neno la kweli na ma million ya watu zaidi ya mainchi 130 katika mikutano na kwenye ma redio na televisheni. Ya wezekana sana sana wandugu wa Bara la Afrika ime kuwa musahada kulingana na ono ambalo ndugu Branham aliona la tai ya Ujerimani ikiruka kwenye Bara la Afrika. Katika inchi zote na katika miji yote nili onyesha nabii na hudma yake lakini nina hubiri Yesu-Kristo kama mkombozi; Ambae ni yeye yule jana, leo na hata milele, na kwa uaminifu, nilihubiri tu neno la Mungu. Sija hwai kufanya mapatano kwa ajili ya neno la Mungu hazarani wala sija wayi kutaja jina la mtu

yeyote kati ya wale wanayo chukuwa mafundisho ya uongo. Kwa sasa kulingana na jinsi watu wameinuwa mwanadamu kupita kipimo kama ibada ya uabudu sanamu inavyo endelea kuwekwa katika matendo kwa watu wa nabii pamoja na picha na misalaba, vipande vya mawe zaidi sana kwa maeneo kama makaburi, etc, ambazo wamezigeuza nafasi za kuwa wanatembelea, kwa sasa nina sina uchaguzi fulani baali kupaza sauti yangu igawa sauti yangu inaweza kusikilikana ao apana. ndugu wa Marekani alie nipokea alinitumia kanda ine na CD. Hizi zilinifikia kwa muda mzuri nilipo kuwa nime kwisha maliza kuandika majibu ya maswali hayo, sikupenda tena kuzirudilia mara tena. Nilipo maliza kupokea kanda hizo nilipata uhakikisho kwa ajili ya wateule kuweka kilakitu kwenye nuru ya kweli ya mambo yaliyo geuzwa na kuya weka kwenye nuru ya neno la kweli la milele. Walifikia hatuwa yakumuweka mahali ambayo haikubaliwe na injili ya milele ya Yesu-Kristo wanasema bila kuacha: „Nabii alisema…“ „Nabii aliniambia…“ na mengineyo na mengineyo

Watu hawa hawamutaje Yesu-Kristo tena. Hata hawanatena sehemu katika hayo ambayo wandugu wanashuhudia. Wanashugulika tu na yale ambayo Nabii alisema nayale ambayo alikuwa akisema akiwazia lakini kuhusu yale ambayo Yesu-Kristo aliyo yasema hawaya jaili tena. Wana jaili tu na maisha ya Nabii, habari zake za kuwinda na mahabari za hema, habari zake za kushika ndege…na mengineyo. Hayo ndivyo yanayo kutaniwa kwa uwingi wa mahubiri na yale ambayo ndugu Branham aliyo yasema kama mwanadamu wanaishuhudia kama; ni **ASEMA BWANA.**

Hii si ndiyo ujao wa kuiacha injili ya kweli ya Bwana wetu Yesu-Kristo kama vile ilivyo hubiriwa na Paulo?(Wagalatia 1). Njia ya upotevu inayo ongoza kwenye ibada ya sanamu? Baada ya miaka makumi ine habari ya maisha yake iliendelea kutangazwa na kuendelea kutokeza maneno mapya! Tuliwai kuwa na habari za maisha ya Yoane mbatizaji, ya Petro ao ya Paulo? Ao tunayo maneno kuhusu maisha ambayo Mungu aliongea kupitia kinywa chao? William Branham alituachia mahubiri ya neno halisi linalo ngaa kama teruji ambalo lina turudisha kwa Mungu.

Ndugu Branham kupitia kinywa chake mwenyewe alihubiri kwamba“kama mtu akikula tunda, anatupa mbegu anaendelea kula tunda“Alisema tena: „unapokula kuku unatupa mifupa“? Ni hayo mambo yanayo fuata yale tunayo ya weka pembeni yote yana fanya

kitu kimoja kile na“mifupa“watu wanabishana. Leo tunapashwa uliza: unaamini ujumbe gani? Ni injili gani unayo yihubiri? Hapo mwanzo kulikuwa neno hakuna tafsiri! Hapo mwanzo kulikuwa umoja, hakuna magawanyiko, mapatano – muchanganyiko hainge wezekana. Kwa mwanzo Mungu alitenganisha nuru na giza na iliendelea hivyo hata milele. Yeyote asiye kubali neno la Mungu la kweli pekee kama yakini yake yeye anasaliti ukweli; na hapo amelaaniwa, na kuhukumiwa kuamini uongo na atahukumiwa (2. Wathesalonike 2:10-12) maneno ya ndugu Branham yaliyo magumu kwetu kuelewa, nayale ambayo yanalingana na hudma yake mwenyewe yanapashwa kuachwa katika mikono ya Mungu. *“mambo ya siri ni ya Bwana Mungu wetu, lakini mambo yaliyo funuliwa niyetu sisi na watoto wetu milele…“* (Kumbukumbu 29:29)

Wandugu wa dunianzima walionesha uzuni yao kuhusu yale yanayo fanyika huko Marekan. Mimi si muhukumu lakini kupitia mwito wangu wa kiungu wa kweli ningependa nioneshe musimamo wangu. Makao makuu yangu hayako hapa Duniani baali yako mbinguni. Na „sauti ya Mungu“ inasikilikana kupitia utangazaji wa neno la Mungu Duniani pote. Maonyo haya ya kimaandiko yangali ya kweli*: „leo kama mtaisikia sauti yake, msifanye migumu mioyo yenu kama wakati wa kukasirisha!“* (Waebrania 3:15) Kama vile manabii wote na Bwana na Mitume kwa wakati wali tumika kazi ya Mungu mahali tofauti hata pia Hudma ya ndugu Branham ilitumika sana katika maskani ya Jeffersonville. Hakuna mtu anapashwa kusafiri kwenda Yerusalemu sasa ingawa neno la Mungu lilitokea huko. (Isaya 2, Matendo 2) Nilikuwa nimekwisha pata mahubiri yote ya ndugu Branham iliyowekwa kwenye kanda mbele ya kusinziya kwake, Nahata hivyo nilikuwa na chakula cha kiroho cha kweli mbele ifunguliwe huko Jeffersonville kama „sauti ya Mungu iliyo wekwa kwenye kanda“. Neno la Mungu lililo funuliwa halikuwekwa chini ya uangalizi wa mwanadamu, ila, liko wazi na kusomwa na kila mtu. Kwangu mimi maandiko matakatifu yata dumu kweli milele, ambamo muna maonyo yafuatayo katika Amosi 5:4-6: *„Nitafuteni mimi nanyi mutaishi baali msitafute betheli wala msiingie Gelgali, wala msipite kwenda Beel-sheba; kwani Gelgali hakika yake itaenda utumwani na Betheli itakuwa ubatili. Mutafuteni Bwana nanyi mtaishi…“* Hizo mahali zote zilikuwa mahali ambazo Mungu alikuwa akijifunua kwa taifa lake, lakini tena baadae ziligeuka kuwa nafasi za upotevu. Yerusalemu mji uliyo chaguliwa na Mungu mwenyewe ulibomolewa mara saba. Na mlima Moria ambapo hekalu la

Mungu lilikuwa limejengwa, wa Islamu waliujenga Musikiti yao ya d'EL ASKA na Dome la mwamba. Wakati Hudma ya Mungu inapotumika mahali Fulani, na fasi hiyo inabaki kuwa ya muhimu sana kwa kazi ya Mungu. Lakini wakati kazi ya Mungu ina malizika hapo, nafasi hiyo inageuka kuwa nafasi ya ibada ya sanamu na mengineyo…na wakati wa mfalme Ezekia wa Islaeli nao pia waliabudu nyoka ya shaba ambao Musa alipanika jangwani na kuleta masadaka. Ezekia hakufanya jambo lingine isipokuwa kuibomoa nyoka hiyo kwa vipande vipande (2. Wafalme 18:1-4).

Leo angelituambia *„Nitafuteni mimi nanyi mutaishi!"* hawezi kusema „Nendeni Yerusalemu ao Jeffersonville" hawezi kusema "fanyeni safari ya kuenda kwenye kaburi ya nabii, nendeni huko Arizona ao kufunga safari kuenda kwenye mlima Sunset" kwa kuwa alisema: *„mwanamke unisadiki; saa inakuja ambayo hamtamuabudu Baba katika mlima huu wala kule Yerusalema, … Lakini saa ina kuja nayo sasa ipo ambayo waabuduo halisi watamuabudu Baba katika roho na kweli…"* (Yohana 4:21-25) Yale ambayo Bwana aliyo yasema kwa wakati wake yataendelea kuwa ya kweli leo hata milele Amina! Amina! Nami nilimjua ndugu Branham kama mtu nilikula pamoja naye kwenye meza moja, nilitembea nae katika gari lake. Aliniambiya maneno ambayo yanajulikana kwa watu wachache, nina wekamabaruwa zake 21 alizo niandikia kutoka kwa mwaka 1958 mpaka 1965. Kwa ombi lake la hapo hapo nilihubiri mara mbili katika maskani yake huko Jeffersonville. Niyeye alie niomba kusema kwa pahali yake katika mukutano wa wafanya Biashara inayo itwa"ujao wa injili „yaani" full gospel"kwa Demos Shakarian kwenye „Cliftonis Cafeteria"ya huko Los Angeles. Ni mambo ambayo nina ya kumbuka kwa furaha. Hata aliniambia jina ya ndugu alie mlipia deni yake ya kodi ya dola 40, 000, kwa kusudi aweze kugomboa vitambulisho vyake yaani"passport"nili kunywa chai kwake nyumbani Baada ya hizo safari zote nilizo zifanya niki mtembelea huko Tucson, nilifanya saa nyingi za usiku katika offisi yake. Lakini sasa habari za maisha yake zina kazi gani kuhusu shahuri za Mungu? Ndugu Branham yeye pia alikuwa mwanadamu. siya kushangaza wakati ya mahubiri, alisema 700 pahali pa 7000, ao kusema kama Henoki alitembea na Mungu muda wa miaka 500 na japo alimaliza miaka 365 hapa duniani. Hiyo inaonesha namna gani mwanadamu anaweza kujidanganya kupitia kwa ulimi wake. Kwa mfano alipo sema "…mbegu zita chomwa…". Badae alijikosoa hiyo akasema."Makapi yata chomwa lakini mbegu zita pelekwa katika gala

la mbinguni „Alipo sema kwamba Noa alihubiri miaka 120, hapo anarudilia maneno ambayo wengine walikuwa wa mesema lakini miaka 120 ndiyo nyakati ambayo Mungu alikuwa ame panga kwa mwanadamu katika (Mwanzo 5:3) Noa alikuwa na ukubwa wa miaka 500, alipozaa watoto wake 3 (Mwanzo 5:32) na alikuwa na 600 wakati garika ilipo fika hapa duniani. (Mwanzo 7:6) Ingawa ndugu Branham alikuwa na Hudma ya kinabii isiyi shindwa kuna maneno machache aliyo yasema ambayo inaonyesha kwamba ni mwanadamu kama wengine. Kwa mfano kama mwanadamu alisema mambo yafuatayo katika mahubiri yake"Unyakuo"akiilinganisha na 1. Wathesalonike 4, ambayo ina sema kuhusu kurudi kwa Kristo Bwana wetu (…mambo matatu ambayo yanastahili kutendeka mbele yakuonekana kwa Bwana mwenyewe): sauti ya agizo, sauti ya malaika mkuu, parapanda ya Mungu…Yesu atatimiza mambo haya matatu atakapo shuka…" Ndugu Branham alitaka sema kwamba mambo haya matatu yatatimia wakati ya Yesu atarudi.*"kwa kuwa twawaambiyeni haya kwa neno la Bwana, kwamba sisi tulio hai tutakaosalia hata wakati wakuja kwake Bwana, hakika hatuta watangulia wao walio kwisha kulala mauti. Kwa sababu Bwana mwenyewe* (sio Ujumbe) *atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko na sauti ya Mungu; nao walio kufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu ili tumlaki Bwana hewani na hivyo tuta kuwa pamoja na Bwana milele"* (1. Wathesalonike 4:15-17). Mambo haya yatatimia kwa siku moja na kwa wakati moja.*"Angalieni na waambia ninyi siri; Hatuta lala sote lakini sote tutabadilika <u>kwa dakika moja kufumba na kufumbua</u> wakati wa parapanda ya mwisho; maana parapanda italia na wafu watafufuliwa, wasiwe na uharibifu, nasi tuta badilika* (1. Wakorintho 15:51-52). Ndugu Branham alisema wazi waazi"kwanza ujumbe unatangulia na sasa ni wakati wakusafisha taa. Amkeni na mkasafishe taa zenu…" Hii siyo 1. Wathesalonike 4, bali ni matayo 25, 6: *„Tazameni Bwana Arusi anakuja ondokeni mwende muka mlaki"*misemwa Fulani isiyo eleweka, mambo yakuunda yanatumiwa kama mafundisho, wakisema kwamba tangu kufunguliwa kwamihuri, Yesu aliacha kiti cha rehema ambacho kimegeuzwa kuwa kiti cha hukumu nayeiko katika"mwendeleo wa kushuka". Hii nimaneno gani ya upuuzi ambayo hayaeleweki!

Mambo mengi yangeliweza kuongelewa kuhusu hiyo lakini tusimamie hapa kwa ajili ya maelezo yafuatayo: katika miaka hii 14ya kwanza tangu mwaka wa 1966, kulikuwa mwenendo mzuri katika ujumbe kwa

mwaka 1979, shetani alijaribu kubomoa kazi ya Mungu na kuuwa ushawishi wa hudma hii. Tangu wakati huo mafundisho ya uongo yote tofauti yaliingizwa. Wandugu wengi hawajui namna gani kumeanza mwanzo mpya, na ginsi gani mwendeleo ya kazi iliendelea tangu wakati ndugu Branham alirudi nyumbani. Ndugu Branham aliona ginsi Bibi arusi alitoka katika hatua lakini tena akaona ginsi anarudishwa tena kwenye hatua kupitia neno.

Wakati yoyote mahubiri yake yaliachwa ginsi yalivyo kuwa, Hapakukuwa magawanyiko hata moja. Magawanyiko yalianza fanyika kwa mwaka wa1980, wakati wandugu walianza kukusanya ma nukuu za ndugu Branham na kuzitosha ma hali pake na hapo walizifanya kuwa mafundisho mapya na kujipatia matumaini ambayo hailingane na maandiko matakatifu. Neno linaturudisha katika inchi ya Ahadi lakini matafsiri yanaturudisha"katika ukiwa" (no man's land).

Kulingana na hali yenye iko kwa sasa tuna weza shuhudia kwamba; hakuna mwana damu anaeweza kutatua shida zilizo katika ujumbe wa mwisho isipo kuwa Mungu mwenyewe. Wote wana sema: „wateule hawawezi danganywa"na ijapo kuwa hata wao wenyewe wame kwisha, wamejidanganya na kudanganya wengine upotevu hauja wai kutoka inje ila unatoka ndani (Matendo 20:30) naniyakushangaza ina karibiyana na ya kweli. Wanaendelesha mafundisho yao binafsi wakiziita kuwa ni ufunuo lakini hauwezi kupata ushuhuda wake katika maandiko matakatifu. Inauzunisha! Lakini kwa kweli ni lazima yale yaliyofanyika katika madhehebu huko mwanzoni ya rudi tena leo katika ujumbe wa wakati ya mwisho. Wana sema"Nabii wao"na"Nabii mke wao"ao waanzilishi wao. Kukirikwawo ni! "Tunaamini Biblia na nabii wetu alisema!"

Ninasema hii tena katika jina la Bwana wetu Yesu-Kristo: musimamo wa kweli ni wa kuheshimu neno la Mungu na kulitambua kama ndilo linalo stahili. Kila Dhehebu imeelewa vibaya na kutafsiri maandiko Fulani za Biblia ambayo yaligeuka kwao kuwa ya muhimu na nikwahiyo madini hayo yamejengwa. Hiyo ndiyo yenye imepatikana ikikutendeka katika ujumbe wa wakati pamoja na Ufunuo 10, kila mafundisho ya uongo yaliyo katika ujumbe wawaki, inakuja katika njia moja ao nyingine kwasababu ya kutoelewa Ufunuo 10, na kuitafsiri vibaya na wameitowa kwa nafasi yake na kuyiweka kwa namna mbaya.

Ndugu Branham ameturudisha kwa musingi ya kimaandiko kwenye kinara na wanatembea kwa hatua moja na neno la Mungu kwa ujao. Hatuamini upofu, ila tuna chunguza katika maandiko ilituona kama mambo tunayo yafundishwa kama ni kweli (Matendo 17:18). Tuna weka vizuri ndugu Branham katika Malaki 4:5-6, kama nabii alie ahidiwa. Alikuwa mjumbe wa kizazi cha mwisho cha kanisa. Amen.

Ni itaji yangu kumutumikia Bwana kwa namna hii iliwale wote wanayo na sehemu ya kanisa bibi-arusi wa Yesu-Kristo warudishwe katika umoja wa Imani. Miaka makumi ine imepita tangu ndugu Branham alichukuliwa katika utukufu na sasa tuna ngojea kurudi na nguvu yaajabu yakitendo cha Mungu ambacho hakija kuweko hapa Duniani. Kupitia uvumilivu, Ayubu ndie mfano wetu katika Biblia alie rudishiwa mara dhufu. Shetani alikuwa ameharibu kila kitu kilicho kuwa karibu naye. Hata muke wake alimgeuka akisema: *„Ungali unasimama kwa musimamo wako? Umulaani Mungu ukakufe"* (Ayubu 2:9). Marafiki wake wa karibu walimujaribu na hawakumuamini tena. Lakini sasa wakati ilifika ambayo Mungu aliongea na Ayubu na Hali yake yote ikabadilika. Ayubu aliwaombea marafiki zake na akarudishiwa maradhufu zaidi ya yale aliyo kuwa nayo mbele (Ayubu 42:10-17). Mfano hii ilituachiwa ikilinganishwa na ahadi ya nvuwa ya kwanza nayamwisho ambayo itatembea na kitendo cha mwisho cha kazi ya Mungu mbele ya kurudi kwa Kristo. Wakati Ayubu alipopata jibu maneno ambayo muke wake alisema pamoja na yale mambo ambayo marafiki wake walimfanyizia hayakukumbukwa tena. Hivyo ndivyo itakavyo kuwa hata na kwetu.*"kwa hiyo ndugu vumilieni hata kuja kwake Bwana…, mume sikia habari ya subira yake Ayubu, mmeuona mwisho wa Bwana ya kwamba Bwana ni mwingi wa Rehema…"* (Yakobo 5:7-11)

Mfano wa pili ni Yusufu alietupwa katika shimo na ndugu zake wenyewe na kufungwa katika jela pasipo kosa kwa ajili ya mwanamke. Hiyo ndiyo njia ya kilindi ambayo angeweza kupitia kwanza mbele kuweza kuwa mgawaji wa chakula kwa ndugu zake wakati wa njala. Hakuwasema vibaya, ila ali waambia*: „Munikaribie na waka mkaribia. Akasema mimi ni Yusufu ndugu yenu ambaye mlimuuzisha kwenda Misri. Basi sasa msihuzunike wala msiudhike nafsi zenu kwa kuniuza huku maana Mungu alinipeleka mbele yenu kuhifadhi maisha ya watu … na sasa si nyinyi mulio nituma huku ila ni Mungu…"* (Mwanzo 45)

Hakungelikuwa Ayubu hatunge lijua kuhusu kurudishiwa kwa maradhufu. Hakunge kuweko Yusufu hatungelikuwa na mfano wa ugawaji wa chakula kwa wakati ya njaa. Hakunge kuwako Yohana mbatizaji, njia ya Bwana hainge weza kutayarishwa. Hakunge kuweko mtume Paulo mataifa hawange weza kupata namna ya kuisikia injili. Hakunge kuweko hudma ya ndugu Branham hakungekuwa ujumbe wa wakati wa mwisho. Ndugu Frank hangelipokea mwito wa hapo hapo na kutumwa, Dunia hainge lijua kuhusu Ujumbe. Kwa maneno haya yote hatuja ongeya kuhusu ma hudma za kanisa ya pahali lakini ni hudma zinazo fungwa hapo hapo kwa yale yaliyo fanyika kuhusu Habari za mpango wa okovu wa Mungu. Kulingana na andiko lililo nukuuliwa kwa mwanzo ya kitabu hiki. Niliandika kitabu hiki ni kiwa na zamiri mzuri kwa hiyo nina watakia wote waachiliwe kutoka katika mitego ya mwovu wawe huru wasiendelee kuwa wafungwa wa matafsiri ya nayo wavutia nyuma yayale ambayo wa nayo yataka. kwa kweli kama vile roho mtakatifu ndie anaetuongoza katika kweli yote (Yohana 16:13), na ni hivyo ginsi Roho za upotevu zinaongoza kwa mafundisho ya uongo inayo toka kwa mwovu. (1Timotheo 4:1) Mwaka wa neema umekuja na kufunguliwa kwa kiungu kwa wafungwa inaendelea tangaziwa kwa wote (Luka 4:17-21) kila mtu anaweza kurudi kwa Bwana na kwa neno lake na kupokea ahadi kulingana na mapenzi ya Mungu (Waebrania 10:35-38).

Kwa neema ya Mungu nita uchukuwa musalaba wangu – Bali si uzito wa kutoelewa na matafsiri – mpaka wakati nitapokea taji la uzima. Nitachukuwa Aibu ya Kristo na Aibu ya ndugu Branham na Aibu yangu mwenyewe mpaka nitakapo ingia katika utukufu. Kulingana na hali ya maisha na mimi nilikubali Aibu kama ilivyo kuwa katika maisha ya watumishi wote waliyo mtumikia Mungu hapa Duniani. Itaji yangu kama ilivyo kuwa itaji ya watumishi wote wa Mungu inaendelea kuwa ya kutumikia taifa la Mungu kupitia utangazaji wa shahuri zote za Mungu pasipo makosa. Mungu aweza kunikubalia hiyo mpaka mwisho wa pumzi yangu ya mwisho. Nina weza kusema mimi mwenyewe yale Bwana wangu na mkombozi angeweza kusema kwake mwenyewe*“mimi nimezaliwa kwa ajili ya haya na kwa ajili ya haya mimi nalikuja ulimwengu ili nishuhudie kweli, kila alie wa kweli husikia sauti yangu.“* (Yohana 18:37) Nina penda kila mutumishi wa kweli wa Mungu kusema hivi,“Nimezaliwa upya kwa neno moja na kwa roho moja kwa matumaini ya nayo ishi ili ni shuhudie ukweli.“ninaweza kusema mbele ya Mungu kama vile mtume Yoane alivyo katika

kweli (1. Yohana 2:21) na kwamba; *„Yule anae jua kweli hutusikia…"* (1. Yohana 4:6) *„…Yule alie wa Mungu husikia maneno ya Mungu…* (Yohana 8:47). Hapo mwanzo kulikuwa neno, Hilo neno ndilo tunalo sasa kwa mwisho. kila mtafsiri yote na maoni ya mtu ni sumu inayo toka kwa muovu anaejionyesha kila wakati kama vile malaika wa nuru kusudi apofushe watu. Kile ambacho Mungu alituma kufanya, kitatimilika kanisa-bibi arusi Duniani pote: Bibi arusi atamlaki Bwana Arusi akiwa tayari wakati atakapo kuja. Nina samba mbele ya Mungu kila nafsi iliyo chaguliwa kuwa na sehemu kwa kanisa bibi arusi, nakuita waliyo chaguliwa kutoka katika kila muvurugano waweze kuji weka kwa mustari wa neno la Mungu ili waifikie umoja wa Imani. Hakuna mtu anae stahili kufanya watu kuwa wafungwa wake katika maeneo tofauti na kuwafanya watumwa ili waiamini matafsiri yake mwenyewe. Bali wafunguliwe na waamini tu yale ambayo maandiko matakatifu yanayo sema. Amen!

*"Na Roho na Bibi – arusi wasema, njoo! Naye asikiaye na aseme, njoo! Naye mwenye kiu na aje; na yeye atakaye, na ayatwae maji ya uzima bure".*

*"Yeye mwenye kuyashuhudia haya asema, naami; naja upesi, Amina; na uje Bwana Yesu. Neema ya Bwana yesu na iwe pamoja nanyi nyote. Amina."* (Ufunuo 22:17, 20-21)